

**MAN CITY YASAKA WALINZI WA KATI**

UKURASA 22

**SERA** mpya yatoa majibu mustakabali kuhusu elimu

UKURASA 4



**WATU** wawili wauawa kwa kutuhumiwa majambazi

UKURASA 5

**TUME** yafanya uchunguzi wa wanaodaiwa kuuawa Pemba

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
Nipashe
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

Jumamosi Januari 11, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581918
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Mbowe: CHADEMA itakuwa imara zaidi



Mbowe

**ASEMA** atakayeshindwa na 'kusepa na kijiji' hatakiyumbisha chama...*Endelea ukurasa wa 2*

## Serikali yataja hatua nane kuboresha uwekezaji

UKURASA 3



## Dk. Slaa akamatwa, ahojiwa na polisi

UKURASA 3

**MICHEZO** HATIMA YANGA ROBO FAINALI AFRIKA LEO UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Dk. Kaushik apata tuzo ya Rais India

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji na Daktari Bingwa wa Hospitali ya Shree Hindu Mandal Dar es Salaam, Dk. Kaushik Ramaiya, amepata Tuzo ya Heshima ya Pravasi Bharatiya Samman 2025 (PBSA) kutoka kwa Rais wa India.

Tuzo hiyo imetokana na mchango wake wa kipekee wa kutoa huduma ya matibabu kwa jamii.

Tuzo hiyo ilitolewa jana katika Mkutano wa 18 wa Pravasi Bharatiya Diwas uliofanyika Bhubaneswar, Odisha unaolenga kushereheka mchango wa diaspora wa India katika nchi wanazoishi.

Kwa mujibu wa taarifa, tuzo ya PBSA ni ya heshima ya juu zaidi inayotolewa na serikali ya India kwa watu wa nchi hiyo, watu wenye asili ya India au mashirika yanayoendeshwa na watu wa India kutambua mafanikio yao makubwa ndani na nje ya nchi.

Dk. Kaushik, raia wa Tanzania mwenye asili ya India, amekuwa akifanya utafiti kwa miaka mingi kuhusu magonjwa yasiyoambukiza, yakiwamo uhimilivu wa sukari mwilini na hatari za magonjwa ya moyo hasa miongoni mwa jamii za Wahindi barani Afrika.

Mtaalamu huyo wa magonjwa ya ndani (Endocrinologist) pia anafanya kazi na watoto wenye ugonjwa wa kisukari aina ya kwanza, kisukari cha ujauzito, dalili za kimetaboliki na matatizo ya moyo yanayotokana na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI.

Pia anashirikiana na Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutekeleza programu za kisukari na magonjwa yasiyoambukiza katika hospitali za kanda, mikoa, wilaya na vituo vya afya Tanzania.

Dk. Kaushik amechapisha zaidi ya makala 100 katika majarida ya kitaaluma na hivi karibuni alichaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Dk. Kaushik ni raia wa nne wa Tanzania mwenye asili ya India kupokea tuzo hiyo. Wengine ni Jayantilal Keshavji Chande (2005), Dk. Rajni Kanabar (2010) na Hajiat Shamim Parkar Khan (2019).

India ni nchi inayotoa diaspora wengi zaidi duniani na ni hazina muhimu kwa taifa. Diaspora wa India wamekuwa wakikuza uhusiano wa kitamaduni na kuimarisha ushawishi wa India duniani kwa kutangaza utamaduni, urithi, mila, na vyakula vyake.

Pia wanachangia kuleta maendeleo ya nchi wanazokaa na kuimarisha mahusiano ya pande mbili. Ili kuheshimu mchango wa diaspora ya India, Serikali ya India imekuwa ikiadhimisha Pravasi Bharatiya Divas kila Januari 9 tangu mwaka 2003.

Mkutano wa Pravasi Bharatiya Divas hufanyika kila baada ya miaka miwili kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya jamii ya Wahindi waishio nje ya India na serikali ya India, huku ukiwapa fursa ya kuungana na mizizi yao ya kitamaduni.

Mwaka huu, Mkutano wa 18 wa Pravasi Bharatiya Divas ulifanyika Bhubaneswar, Odisha kuanzia Januari 8 hadi 10, 2025, ukiwa na kaulimbiu "Mchango wa Diaspora kwa Bharat Ilioendelea.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Balozi wa Marekani nchini, anayemaliza muda wake, Michael Battle, katika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Mbowe: CHADEMA itakuwa imara zaidi

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amekoleza joto la uchaguzi ndani ya chama hicho kwa kusema mgombea atakayeshindwa na kuamua kuhama, atakiacha kikiwa imara.

Mbowe ambaye anatetea nafasi yake ndani ya CHADEMA, anachuana na Makamu wake (Bara), Tundu Lissu, kwenye uchaguzi uliopangwa kufanyika Januari 21, mwaka huu.

Akihojiwa jana na kituo kimoja cha redio mkoani Dar es Salaam. Mbowe alisema chama hicho ni taasisi kubwa kuliko kiongozi na mgombea yeyote na kwamba madai ya mgombea kushindwa kwenye uchaguzi na 'kusepa na kijiji', hayana nguvu ya kukipasua.

"CHADEMA ni kubwa kuliko Lissu. Ni kubwa kuliko Mbowe. Hiki chama kimebeba matumaini ya mamilioni ya Watanzania wanaotumaini kitaleta mabadiliko katika nchi hii. Kila mmoja ana wafuasi kwa nafasi yake. Nguvu ya kila mmoja ndani ya CHADEMA inatokana na umoja wetu.

"Yeyote anayefikiri atasepa na kijiji kama wanavyosema vijana wa mjini, atachoka sana. Yeyote anayefikiri akiondoka CHADEMA itameguka... sikiliza, kuna watu 300 hapa Dar es Salaam wanaomba nafasi za uongozi. Kuna watu wanasema CHADEMA itakufa kama TLP na NCCR-Mageuzi. Hivyo vyama vilikuwa bado vichanga mno ndiyo maana walioondoka walivipasua," alisema.

Mbowe alisema chama hicho kimeweka mizizi nchini nzima kwenye mabaraza yake ya Vijana (BAVICHA), Wanawake (BAWACHA) na

Wazee (BAZECHA) na kina wanachama kuanzia ngazi ya vijiji.

"Tuna mamilioni ya wapigakura. Tumejijenga na hiki chama ni taasisi. Chama cha kidemokrasia kilichojengwa kama CHADEMA hakiwezi kudhoofishwa na mtu mmoja. Siamini kwamba kuna mtu akitoka CHADEMA chama kitapasuka. Siamini kama wanachama wa CHADEMA wapo kwa sababu ya sura zetu sisi viongozi. Naamini wapo kwa sababu ya malengo ya pamoja ambayo tumeamua kuyapigania," alisema.

Alisema hana ugomvi na Lissu wala mgombea yeyote ndani ya CHADEMA na minyukano inayoendelea inamsikitisha.

"Lissu nina historia ndefu naye. Ninakaa namwangalia Lissu ambaye nimekaa naye, nimefanya naye kazi, nimeshirikiana naye kifamilia, kisheria, kisiasa, kibunge, halafu anatoa kauli dhidi yangu, kweli kibinadamu hainipendezi. Najipa uvumilivu sana kuvumilia jambo hili.

"Namwomba sana Mungu anisaidie nisijenge chuki na kisasi juu ya haya kwa sababu yanapita; nafunga sana, naomba Mungu atuvushe salama, lakini zaidi ya yote, nisibaki na chuki na mtu," alisema na kuongeza kuwa kitendo cha viongozi wakuu kugombea nafasi ya uenyekiti kinatafsiri kwamba mafahali wawili hawakai zizi moja.

Alisema hata yeye (Mbowe) akishindwa kwa haki haitakuwa shida kwake kwa kuwa anaamini katika mchakato wa kidemokrasia ambao chama hicho kimeujenga. Alisema ikiwa atashinda, ataendelea kufanyakazi na Lissu pamoja na wanachama wengine.

"Si Lissu tu na wengine wengi walioshindwa katika ngazi mbalimbali tunawahitaji, tunahitajiana pamoja na tofauti zetu. Pamoja na mapungufu yetu bado tunahitajiana," alisema.

Alisema wanaosema 'Mbowe must go' wanapaswa kutambua kwamba chama hicho kinahitaji hadi walio nje na kwamba kuna maisha baada ya Januari 21. Alisema dhana ya uongozi wa kisiasa inakwenda na malengo ya pamoja kama mchezo wa mpira wa miguu unaohitaji nguvu ya pamoja na kushinda.

Mbowe alisema CHADEMA imefika kuwa taasisi imara kwa kujengwa na Watanzania wengi wakiwamo wasio wanachama na kwamba minyukano inayoendelea ndani ya chama hicho ni kutokana na ukubwa na mafanikio kilichopata kwa muda mrefu.

**MABADILIKO YA KATIBA**

Kuhusu mabadiliko ya katiba ya chama hicho kuweka ukomo wa uongozi, alisema ni mchakato unaoweza kuchukua muda mrefu kwa kuwa baada ya kupita ngazi mbalimbali, inafikishwa kwenye mkutano mkuu ambao hufanyika mara moja katika kipindi cha miaka mitano.

Mabadiliko ya katiba ya CHADEMA ni moja ya agenda ya Lissu ambaye amesema akiingia madarakani ataifumua na kuisuka upya ili pamoja na mambo mengine, kuweka ukomo wa uongozi.

Kuhusu kumtuma Mwenyekiti wa Kanda ya Victoria, Ezekiel Wenje, Mbowe alisema ni uzushi na propaganda kumhusisha na mgombea yeyote kwa kuwa kila mwanachama mwenye sifa ana haki ya kugombea uongozi.

**KAMATI KUU**

Baada ya mahojiano na Clouds Media, Mbowe alihudhuria kikao cha Kamati Kuu ya CHADEMA, ambacho kilikuwa kinaongozwa na Lissu kwa muda.

Baadhi ya wajumbe waliohudhuria kikao hicho ni John Heche anachuana na Wenje kwenye nafasi ya Makamu Mwenyekiti (Bara), ambaye anamuunga mkono Lissu.

Lissu na Mbowe kama kawaida, jana walikaa pamoja wakati wa kikao hicho, kilichofanyika makao makuu ya CHADEMA, Mikocheni mkoani Dar es Salaam.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Elimu Taaluma wa Jiji la Dodoma, Issa Kambi (kushoto) na Msimamizi wa kituo cha upimaji wa watoto wenye ulemavu, Neema Mkama (katikati), wakizungumza na mzazi aliyefika kumwandikisha mtoto wake, katika kituo cha Shule ya Msingi Nkuhungu, Kata ya Chamwino, jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yataja hatua nane kuboresha uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeainisha hatua nane za kuboresha uwekezaji nchini ikiwamo kutoa vibali kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi kufungua vituo vya uhamasishaji uwekezaji na kuanza kutekeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo maalum ya kiuchumi ikiwamo Bagamoyo.

Aidha, kwa mwaka 2025, serikali imejiwekea lengo la kuvutia miradi mipya 1,500 ya uwekezaji na mitaji ya Dola za Kimarekani bilioni 15 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Sekta mahsusi ni viwanda, kilimo, uchukuzi, nishati safi, utalii, madini na huduma, ongezeko litakaloifanya Tanzania kuwa moja ya nchi tano bora katika uwekezaji barani Afrika kwa wingi wa mitaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, jana alikuwa akitoa mwenendo na hali ya uwekezaji nchini katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya sita ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa akizungumza na wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari nchini.

Hatua zingine zilizoainishwa ni kutunga Muswada wa Sheria Mpya ya Uwekezaji Tanzania ambao pamoja na mambo mengine, unapendekeza kuunganisha taasisi za TIC na EPZA. Muswada huo uliwasilishwa Bungeni mwaka 2024 na sasa uko katika ngazi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Aidha, kuandaa awamu ya pili ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI). Ni baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa MKUMBI I uliobaini mafanikio mbalimbali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Pia, tathmini hiyo ilibaini changamoto mpya zilizojitokeza ambazo serikali na wadau wanaendelea kuzifanyia kazi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye mazingira bora ya kufanya biashara na uwekezaji barani Afrika. Hatua zingine alizozitaja ni kuanzisha utaratibu wa kuzipima mamlaka za serikali za mitaa katika kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji. Kuanza kutekeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo maalum ya kiuchumi ikiwamo Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone) ili kuwezesha ujenzi wa viwanda.

Prof. Mkumbo pia alisema serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani ukiwa na lengo la kufikisha asilimia 50 ya miradi yote ya uwekezaji kwa mwaka imilikiwe na Watanzania.

"Tutashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kuwalenga wawekezaji wa ndani hasa wawekezaji wadogo wanaokua. Kuboresha na kuwezesha ofisi za sekretarieti za mikoa katika kuhudumia na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika ngazi na mikoa na wilaya nchini kote.

"Kwa mwaka 2025, tutaanza na kufungua ofisi ya Kanda ya TIC mkoani Njombe ili kusogeza huduma za uwekezaji mkoani Njombe, Iringa na Ruvuma," alisema.

**MIRADI ILIYOSAJILIWA 2024**

Prof. Mkumbo alisema hadi Desemba, 2024, TIC ilikuwa na miradi 13,282 ya uwekezaji iliyosajiliwa na kutekelezwa nchini, ikivutia mitaji kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 127,176 na kutoa ajira zaidi ya milioni 1.98.

Alisema mafanikio katika sekta ya uwekezaji yamechochewa na sababu mbalimbali ikiwamo kuendelea kuimarisha mifumo ya kisera na sheria katika kuwezesha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, maono, hamasa na ushawishi ambao umeendelea kufanywa na Rais Samia kwa kampuni mbalimbali za kimataifa kuja kuwekeza nchini kupitia ziara na mikutano mbalimbali aliyoifanya nje na ndani ya nchi.

Pia kampeni kubwa ya kitaifa ya uhamasishaji uwekezaji nchini iliyofanyika mwaka jana kwa ushirikiano mkubwa katika ya TIC, chemba za biashara nchini (TCCIA, TWCC), benki, na vyombo vya habari. Jumla ya wafanyabiashara 1,800 walifikiwa kupitia kampeni hiyo katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Kadhalika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, TIC ilisajili miradi 901 ikilinganishwa na 526 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

**WAWEKEZAJI 7 WATIA FORA**

Aliwataja wawekezaji saba wanaofanya vizuri kuwa ni pamoja na Hoteli ya Southern Sun, iliyowekeza Dola za Kimarekani milioni 2.7, Kunduchi Mall, iliyowekeza Dola milioni 20, ujenzi majengo ya makazi na biashara, Dola milioni nne, Kiwanda cha Tumbaku, Dola milioni sita na DP World, iliyowekeza Dola milioni 200.

**MIKOA 5 KUVUTIA WAWEKEZAJI**

Prof. Mkumbo aliitaja mikoa hiyo na wawekezaji kwenye mabano kuwa ni Dar es Salaam (356), Pwani (166), Arusha (64), Dodoma (47) na Mwanza (36).

Aidha, kuanzia Januari hadi Desemba 2024, miradi 901 ilisajiliwa na kuzalisha ajira zaidi ya 200,000.

# Dk. Slaa akamatwa, ahojiwa na polisi

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limethibitisha kumshikilia mwanasiasa mkongwe, Dk. Willibrod Slaa, kwa mahojiano.

Taarifa hiyo ya polisi imetolewa baada ya kusambaa taarifa kuwa alikamatwa juzi akiwa anafanya mazoezi karibu na nyumbani kwake, Mbweni mkoani Dar es Salaam.

Aidha, ilisambazwa sauti inayoelezwa kuwa ni ya Dk. Slaa akieleza kuwa amekamatwa na Jeshi la Polisi na anapelekwa Kituo cha Polisi cha Mbweni.

"Nawajulisha tu kwamba kuna polisi wamenifuata, nitawajulisha kitakachotokea, napelekwa Mbweni kituoni," Dk. Slaa alieleza.

Alizungumza na Kituo cha Redio cha Wasafi FM jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema ni kweli wanamshikilia Dk.Slaa kwa mahojiano.

Alisema wakati wanaendelea kuhoji wataangalia maelekezo ya mifumo ya kisheria kisha hatua zingine zitafuata.

"Ni sahihi daktari yupo, tuko naye na tumekuwa na mahojiano naye kwa baadhi ya mambo na mahojiano yetu yanakwenda vizuri. Kwa hiyo tunaangalia mifumo ya kisheria inatuelekeza nini cha kufanya. Naamini taarifa zaidi zitatolewa baadaye," alisema Kamanda Muliro.

Hata hivyo, jana majira ya saa 8:00 mchana, taarifa zilizodai kuwa Dk. Slaa amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, zilienea kwenye mitandao ya kijamii.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X, mwanaharakati Mdude Nyagali, alisema alipata taarifa kuwa Dk. Silaa alifikishwa kwenye mahakama hiyo.

"Nimejulishwa kwamba baada ya Dk. Slaa kufichwa tangu asubuhi, muda huu amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Tayari mawakili wetu wanaelekea hapo," alisema.

# Tanzania yasifu Marekani kwa misaada ya maendeleo

**Na Benny Mwaipaja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Tanzania inathamini mchango mkubwa wa Marekani katika maendeleo ya nchi kupitia miradi na programu mbalimbali zinazofadhiliwa na nchi hiyo.

Miongoni mwa programu hizo ni mkataba wa msaada wa dola za Marekani bilioni 1.14, uliotiwa saini hivi karibuni kwa ajili kuendeleza sekta mbalimbali.

Dk. Nchemba aliyasema hayo jijini hapa jana wakati akiagana na Balozi wa Marekani aliyemaliza muda wake wa uwakilishi Tanzania, Michael Battle. Waziri na balozi huyo walitumia fursa hiyo kujadili maeneo mapya ya ushirikiano kati ya Tanzania na Marekani hususan katika biashara na uwekezaji.

"Ninashukuru kwa msaada wa Dola za Marekani bilioni 1.14 uliotolewa na taasisi za Marekani kupitia programu ya Development Objectives Agreement (DOAG), unaoonesha namna Marekani inavyochangia maendeleo ya nchi yetu.

"Fedha hizo zitaelekezwa kwenye sekta za afya, elimu, kukuza uchumi na utawala bora, hivyo kuchangia Agenda ya Dira ya Taifa ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26," alisema Dk. Nchemba.

Dk. Nchemba alirejea pia shukrani zake kwa Marekani kwa kuipa nafasi Tanzania ya kuboresha masuala kadhaa kupitia Mradi wa Millenium Challenge Corporation (MCC), ili nchi irejee kwenye mpango mkuu wa maendeleo na kwamba serikali imeimarisha kwa kiasi kikubwa misingi ya demokrasia, haki za binadamu, utawala bora pamoja na maendeleo ya nchi.

Balozi Battle alisema Marekani na Tanzania ni washirika wa muda mrefu wa maendeleo na kwamba uhusiano huo umeendelea kudumishwa na kuimarishwa hadi sasa.

Battle aliyeambatana na Naibu wake, Andrew Lentz, alisema ushirikiano huo unatarajia kuchukua mwelekeo mpya kwa kuhimiza zaidi biashara na uwekezaji kwa faida ya pande zote mbili hususan kwa kutumia ukanda wa kibiashara wa Bahari ya Hindi pamoja na uwepo wa fursa ya gesi (LNG).

Aidha, alisema Marekani inaandaa mpango mpya wa kutumia Sheria ya ukuaji wa fursa Afrika (AGOA) unaolenga kukuza masoko na biashara ndani na nje ya Marekani, ambapo mwelekeo utakuwa ni ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi na nchi (bilateral) badala ya Marekani na mataifa mengi kwa pamoja (Multilateral).

Mazungumzo ya kuagana na Balozi Battle, yalimhusisha pia Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Amina Khamisi Shaaban, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.



Raia wa Watanzania walioenda Afrika Kusini kinyume cha sheria, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kulipa faini ya elfu 40 au kifungo cha miezi sita jela kwa kila mmoja. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Sera mpya yatoa majibu mustakabali wa elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na mitaala ilivyoboreshwa ambayo inatoa majibu ya hoja mbalimbali za wadau ikiwamo lugha ya kufundishia na matumizi ya Akili Mnemba (AI).

Akizungumza jana jijini hapa kuhusu uzinduzi huo utakaofanyika Januari 31, mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema mageuzi yaliyomo kwenye sera ni makubwa na yanatekelezwa kwa awamu na kila mwaka yatakuwa yanaonekana.

"Ni mabadiliko ambayo yanagusa vizazi na vizazi, ukamilifu wa utekelezaji wake kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita utachukua muda, kwa sababu tumeanza hatua kwa hatua, elimu ya awali, darasa la kwanza, la tatu, kidato cha kwanza," alisema.

Alisema hatua hiyo ni kubwa na itabadilisha mwelekeo wa nchi katika suala la elimu.

"Tunasikia watu bado wanatoa mchango kuhusu maboresho ya elimu. Kuna hoja mbalimbali ambazo zinazungumzwa na sisi tunazifuatilia. Yako majibu ya hoja zote katika sera na mitaala mipya," alisema.

Alitolea mfano miongoni mwa mambo yenye mjadala mkubwa yanayoendelea kwa sasa ni kuhusu somo la Kiingereza ambalo kwenye sera suala la lugha limo na kwenye mitaala ni ufundishaji wa lugha.

"Tunasikia watu wanazungumza suala la 'Artificial Intelligence' ni suala kubwa sana. Ukienda kwenye sera utaona masuala ya TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano) na mambo yote ya TEHAMA yaliyozungumzwa na ukija kwenye mitaala utaona utekelezaji wake unavyofanyika,"alisema.

**"Tunasikia watu bado wanatoa mchango kuhusu maboresho ya elimu. Kuna hoja mbalimbali ambazo zinazungumzwa na sisi tunazifuatilia. Yako majibu ya hoja zote katika sera na mitaala mipya," alisema.**

Kadhalika, alisema suala la sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati linazungumzwa sana na kwenye sera inabainisha namna inavyozingatiwa na mitaala inaeleza namna inavyotekelezwa.

"Kuna masuala ya kumwandaa mwanafunzi, sio tu kwenye ubora wa elimu lakini kuwa na ujuzi unaomwandaa kwenye dunia ya sasa na mabadiliko makubwa yanayotokea duniani, kwenye sera utaona masuala hayo yanavyoshughulikiwa na kwenye mitaala utaona jinsi yanavyotekelezwa," alisema.

Alisema wadau na viongozi mbalimbali wamealikwa kwenye uzinduzi huo unaotarajiwa kuhudhuriwa na watu takribani 3,000 na kutakuwa na maonesho ya taasisi mbalimbali za elimu.

Awali, alifafanua kuwa Rais Samia alipohutubia Bunge alitoa ahadi kwa Watanzania kwamba serikali anayoiongoza itahakikisha inafanya mageuzi makubwa ya sera ya elimu na mitaala.

"Kutokana na ahadi hiyo alitoa maelekezo mahsusi kwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kusukuma jambo hili, na baada ya maelekezo ya Rais wetu kazi ilianza ya kufanya mageuzi, mapitio ya sera na mitaala na kazi hii imechukua takribani miaka mitatu," alisema.

Prof. Mkenda alisema kazi hiyo imefanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwamo wataalamu wa elimu, walimu, wanafunzi, wananchi na maoni yalipokelewa nyakati zote ili kuleta ufanisi kwenye mapitio hayo.

Pia alisema mchakato huo ulihusisha kujifunza kwenye nchi mbalimbali na walitembelea kwenda kuangalia wanachofanya kwenye elimu ili kupata mbinu za kuboresha elimu ya Tanzania.

"Kazi ya kupitia sera imekamilika na sasa tunayo sera ya elimu hapa nchini ambayo inaitwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023, na tayari imeshaidhinishwa na Rais kupitia kikao cha Baraza la Mawaziri, Mitaala pia imefanyiwa mapitio na kubadilishwa kuendana na sera ambayo tunayo," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sera hiyo, serikali imeanza kuwapiga msasa walimu nchi nzima na inataajiri hivi karibuni walimu 4,000 wa somo la biashara.

Naye Naibu Waziri, Omar Kipanga, alisema jambo hilo ni kubwa na ni kiu ya watanzania kuona mageuzi hayo katika mfumo wa elimu nchini.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo, alivishukuru vyombo vya habari namna vinavyotoa taarifa kwa umma kuhusu mageuzi yanayofanywa na wizara hiyo na inavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# Diplomasia ya Samia kuwaleta wakuu wa Afrika mkutano mkubwa wa nishati

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ujulikanao kama Mission 300 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo diplomasia ya kiuchumi chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jana alipozungumzia Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika utakaofanyika Januari 27 na 28, mwaka huu, utakaofanyika jijini Dar es Salaam.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania kimataifa. Hii imesababisha taasisi za kimataifa, kampuni na wawekezaji kuona Tanzania kuwa sehemu sahihi ya kufanya biashara na uwekezaji.

"Mfano halisi ni Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika kuichagua Tanzania kufanya mkutano huu mkubwa wa kimataifa utakaohudhuriwa viongozi kitoka nchi 54 barani Afrika," alisema Dk. Biteko.

Alisema sababu nyingine kubwa ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwa wananchi suala linaloendana na ajenda ya mkutano huo ya kuharakisha kupeleka umeme kwa wananchi milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

"Taifa limepiga hatua kubwa katika sekta ya nishati. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa msukumo mkubwa anaotoa katika sekta ya nishati. Taifa lina umeme wa kutosha na wa ziada na uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1,470 hadi megawati takriban 3,077," alisema.

Dk. Biteko alisema upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwa na iko zaidi ya asilimia 78.

Kuhusu mafanikio ya sekta ya nishati, Dk. Biteko alisema vijiji vyote 12,318 Tanzania sasa vimesambaziwa umeme na tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia barani Afrika mwaka jana, imeonesha kuwa Tanzania iliongoza kwa kusambazia wananchi umeme vijijini.

Dk. Biteko alisema baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji na katika vitongoji 64,000 nchini, takriban 36,000 vimepelekewa nishati hiyo.

Alitaja faida za mkutano wa M300 kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuongeza fursa za kupata fedha za kuendelea na miradi mbalimbali, kuongeza fursa za uwekezaji, kupata uzoefu kutoka kwa waliofanikiwa zaidi kwenye sekta ya nishati na kuongeza heshima ya nchi kimataifa.

Faida nyingine, alisema ni kuharakisha upatikanaji umeme nchini na wananchi watakaounganishiwa umeme kupitia M300 ni milioni 8.3 ifikapo 2030, hivyo kuifanya Tanzania kuunganisha wateja milioni 13.5 kufikia 2030 kutoka milioni 5.2 ya sasa.

# Wawili wauawa kwa kushukiwa majambazi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limethibitisha kuua watu wawili wanaodaiwa kuwa ni majambazi, katika jaribio la kuiba nyumbani kwa mfanyabiashara, wakiwa wamevalia mavazi ya kike kuficha jinsia na mwonekano wao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilbrod Mutafungwa, alithibitisha jana kuwa watu hao ambao ni wanaume, waliuawa kwa risasi na polisi waliokuwa katika doria juzi saa 2:45 usiku.

DCP Mutafungwa alisema tukio hilo lilitokea katika Mtaa wa Kabambo, Kata ya Kiseke wilayani Ilemela na watu hao walikuwa wamevalia magauni na vilemba.

Alisema walivamia nyumbani kwa Flora Sungura Abdallah (42) na kuingia ndani wakati mfanyabiashara huyo anafunguliwa geti akitoka kwenye shughuli zake za kibiashara.

"Watu hao walikuwa na bunduki aina ya Shotgun moja iliyotengenezwa kienyeji ikiwa na risasi mbili na mapanga mawili. Baada ya hali hiyo, wakazi wa eneo hilo walipiga kelele za kuomba msaada na taarifa hizo kufika kwa askari polisi waliokuwa doria eneo hilo," alisema.

Kamanda Mutafungwa alisema baada ya askari kufika eneo la tukio kwa ajili ya kutoa msaada na kuwataka watu hao kujisalimisha, walikaidi amri na kutaka kuwadhuru wakazi wa nyumba hiyo pamoja na askari.

"Ndipo askari walifyatua risasi, hivyo kusababisha watu wawili ambao mmoja alishika bunduki na mwingine akiwa na panga kujeruhiwa kwa risasi hizo na kupoteza maisha papo hapo," alisema.

Kamanda Mutafungwa alisema miili ya watu hao ambayo haijatambuliwa imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando ikisubiri utaratibu wa utambuzi na uchunguzi wa kitaalamu. Alisema katika tukio hilo hakuna mali iliyoibwa na kuwa jeshi hilo likakamata silaha aina ya shotgun moja, mapanga mawili na begi la mgongoni likiwa na suruali, shati, bisibisi na viatu.

# THBUB yachunguza mauaji Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesema inachunguza vifo vya watu wawili vilivyotokea hivi karibuni, mkoa wa Kaskazini Pemba.

THBUB imesema imepokea kwa masikitiko makubwa vifo vya Athuman Hamad Athuman na Amour Khamis Salim, waliokuwa wakazi wa kijiji cha Kiungoni, Wete, Pemba vilivyotokea Desemba, 2024.

Akitoa tamko la tume hiyo kwa waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali jana, ofisini kwake Mbweni, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi, Kamishna wa Tume hiyo Zanzibar, Khatib Mwinchande, alisema tukio la mauaji hayo ni ukiukwaji wa haki ya kuishi kama ilivyotamkwa na Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 13(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinachoeleza kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kwenye jamii kwa mujibu wa sheria, hivyo tume imelaani vikali vitendo hivyo.

Pia aliizungumzia taarifa kwa umma iliyotolewa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba ya Desemba 25, 2024 iliyoeleza jeshi hilo linaendeleza uchunguzi wa vifo vya watu hao waliofariki dunia wakati wakipatiwa matibabu kwenye Hospitali ya Ali Khamis Camp, Vitongoji Pemba.

Kamishna Mwinchande alibainisha kuwa mauaji hayo ya Kiungoni Pemba yametokea wakati THBUB inaendelea na kazi ya kufuatilia mauaji ya Kidoti, Kaskazini Unguja na matukio mengine kama hayo kwa upande wa Tanzania Bara ambayo yanarudisha nyuma juhudi za serikali za Muungano na za Zanzibar za kuimarisha ulinzi, amani na usalama wa raia na mali zao nchini.

Kamishna Mwinchande pia alisema taarifa za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, zilidai kwamba wakati wa uhai wao, watu hao walichukuliwa na askari wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya wakiwa wazima kwa tuhuma za kuhusishwa na wizi wa baskeli na matumizi ya bangi lakini walirejeshwa siku ya pili wakiwa wamefariki dunia.

Alibainisha kuwa mauaji hayo ni ukatili dhidi ya binadamu na ni kinyume cha Ibara ya 13(6)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 13(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Pia alisema mauaji hayo ni ukiukwaji wa haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru kama ilivyotamkwa kwenye Ibara ya 15(1)(2) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Akizungumzia utawala bora, Kamishna Mwinchande amesema mauaji hayo ni ukiukwaji wa msingi wa utawala bora hususan utawala wa sheria.

Pia alieleza dhamira ya THBUB ya kufanya uchunguzi wa tukio hilo na kuendeleza uchunguzi kwa matukio mengine kama hayo, ni kulinda misingi ya utawala bora na utawala wa sheria nchini.

Kadhalika, Kamishna Mwinchande alitoa wito kwa wananchi na jamii, kutoa ushirikiano kwa THBUB na vyombo vyengine vya uchunguzi vinavyochunguza tukio hilo.

"THBUB inawakumbusha wananchi na taasisi zote, umuhimu wa kupiga vita vitendo vyote vinavyokiuka sheria, ukiukwaji wa misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu, kwa kuwa haki ya kuishi ni haki ya msingi kwa kila mtu," alisema.

Katika hatua nyingine, Mwinchande alitoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Athuman Hamad Athuman na Amour Khamis Salim kwa msiba mzito wa kuondokewa na wapendwa wao kwa njia hiyo na kuwaomba kuwa watulivu na wenye subira hususan wakati huu ambao vyombo husika vinaendelea na uchunguzi wa matukio ya mauaji.

Athuman alifariki dunia akiwa na miaka 75 na Amour alifariki dunia akiwa na miaka 28 na wote walikuwa wakazi wa Kimango Kiungoni, Wete Pemba.

Walidaiwa kukamatwa na maofisa wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika barabara ya Bibi Titi Mohamed, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wasiosajiliwa kuchakata taarifa binafsi waonywa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TUME ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPC) imezitaka taasisi zote za umma na binafsi zinazotoa huduma ya kukusanya na kuchakata taarifa binafsi kujisajili kabla ya Aprili 30, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dk. Emmanuel Mkilia, alitoa agizo hilo jana wakati alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa.

Dk. Mkilia alizitaka taasisi hizo kuhakikisha zinajisajili kwenye tume hiyo kabla ya Aprili 30, mwaka huu, na baada ya hapo zitachukuliwa hatua za kisheria zile ambazo hazitajisajili.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 14 na 21 cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, taasisi zote za umma na binafsi zinazokusanya, kuchakata au kuhifadhi taarifa binafsi zinatakiwa kusajiliwa na tume yetu," alisema.

Alibainisha kuwa awali muda uliopangwa na serikali wa kujisajili wa hiari ilikuwa mwisho Desemba 30, 2024 hivyo wameona waongeze muda wa miezi minne.

Dk. Mkilia alisema tume hiyo inatambua juhudi za taasisi ambazo zimesajiliwa lakini wamebaini bado kuna idadi kubwa ya taasisi ambazo hazijasajiliwa.

Alitaja idadi ya taasisi zilizosajiliwa hadi Desemba 30, mwaka jana, kuwa ni 1,687 kati ya hizo ambazo hazijakamilisha usajili ni 1,472.

Aliongeza kuwa taasisi zitakazoshindwa kukamilisha ujisajili baada ya muda huo zitachukuliwa hatua kali za kisheria zilizowekwa kwa mujibu wa tume hiyo.

Pia alisema kuanzia Mei Mosi, mwaka huu, PDPC kwa kushirikiana na vyombo vya dola, zitazichukulia hatua za kisheria taasisi zote ambazo hazijasajiliwa.

Alisema tume itaendelea kutoa elimu, maelezo na miongozo kwa umma na taasisi zinazofanya mchakato wa usajili.

Dk. Mkilia alisema jukumu la kulinda haki ya taarifa binafsi linatakiwa kuzingatiwa ili kuendeleza heshima ya utu wa mtu.

Hata hivyo, alisema serikali imeweka utaratibu wa kujisajili kwa njia ya kidijitali ili kupunguza usumbufu wa wahusika kusafiri mbali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga pambaneni kwa ajili ya Taifa

**HII** ni wikiendi nzito kwa wadau wa soka na mashabiki wa klabu za Simba na Yanga ambazo zote zipo ugenini kusaka nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano ya kimataifa ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Simba, ambayo inashiriki Kombe la Shirikisho Afrika ipo nchini Angola kwa ajili ya mchezo wao wa kesho wa michuano hiyo dhidi ya Bravo do Maquiz ya nchini humo.

Watani zao wa hapa nyumbani, Yanga wenyewe wapo Maritania kucheza na Wasudan, Al Hilal na wenyewe wakisaka pointi tatu zitakazowasogeza karibu kabisa na mlango wa kuingia robo fainali ya michuano hiyo.

Kwa hapa nyumbani mashabiki wa klabu hizo wanasubiri baada ya dakika 90 kwa kila mchezo kuanza kutambiana na kuchekana kwa kile kitakachotokea kwenye michezo hiyo.

Kimsingi klabu hizi zote zinaipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na CAF, kufanya vizuri kwa klabu hizo ni sifa kwa Ligi yetu na nchi kwa ujumla.

Kutokana na namna ya misimamo katika makundi ya timu hizi kwenye michuano hiyo ya CAF ilivyo, kila timu ina nafasi ya kusonga mbele, kikubwa ni kuchanga vyema karata zao.

Tunaamini kila timu ikipambana kikamilifu, wachezaji wakajitoa dakika zote 90 huku wakiweka malengo ya kupata ushindi, hakuna kitakachoshindikana.

Yanga hawapaswi kuangalia matokeo ya timu nyingine, cha kwanza ni lazima washinde kwanza mchezo wao wa kesho kabla ya kuanza kufikiria mchezo wao wa mwisho dhidi ya MC Alger ambao utachezwa kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa.

Wachezaji wa Yanga wanapaswa kupambana hasa ndani ya uwanja kwenye mchezo wa kesho kuweza kupata ushindi muhimu ambao utaweka hai matumaini yao ya kutinga kwa mara ya pili mfululizo hatua ya robo fainali.

Uwezo wa kufanya hivyo Yanga wanao kikubwa ni kujituma uwanjani katika dakika zote huku pia wachezaji wakifuata maelekezo ya kocha wao.

Kama ilivyo kwa Yanga, Simba nao wana nafasi hiyo ya kupata ushindi na kukata tiketi ya kuingia hatua ya robo fainali Kombe la Shirikisho Afrika.

Utofauti wao na Yanga kutokana na msimamo wa makundi yao, Simba ikipata ushindi kwenye mchezo wa kesho watakuwa wamekata tiketi moja kwa moja kucheza robo fainali bila kusubiri mchezo wao wa mwisho dhidi ya CS Costantine.

Ikumbukwe Simba ina pointi tisa sawa na vinara CS Costantine ambao wao watakuwa wanacheza na 'vibonde' wa kundi, CS Sfaxien, matokeo zaidi ya ushindi yatawafanya Simba nao kusubiri mchezo wao wa mwisho kujua kama watatatinga hatua hiyo ya robo fainali.


Hakuna kinachoshindikana kwenye soka, inawezekana Tanzania ikawa na timu mbili kwenye michuano miwili tofauti katika hatua ya robo fainali.

Kikubwa tunachosisitiza na kushauri, wachezaji wapambane kesho kwa dakika zote tisini kuhakikisha wanapata ushindi huo muhimu ili waweze kutinga robo fainali.

Nipashe tunazitakia kila la heri timu zote tukiamini zinaiwakilisha Tanzania kwenye michuano hii ya CAF, hii itatoa faida kwa Ligi yetu kuzidi kupanda viwango vya ubora miongoni mwa Ligi za Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kilimanjaro Stars imetupa somo wachezaji wazawa na kigeni

**NADHANI** sasa tutaanza kuelewana taratibu juu ya wachezaji wazawa na wa kigeni kwenye ligi yetu.

Umekuwa ni mjadala usioisha, kuhusu kupunguza idadi ya wachezaji wa kigeni, waendelee kuwa 12, au waongezwe.

Kuna baadhi wanataka wapunguzwe kabisa, wawe angalau watano au watatu tu ili kulinda vipaji vya wachezaji wazawa.

Hawa wanaona kuwa wachezaji wa Kitanzania hawapati nafasi ya kuonekana kwa sababu kuna idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni.

Mawazo yao ni kwamba wachezaji wazawa wakipata mechi nyingi sana za kucheza watakuwa kwenye viwango vya hali ya juu na kuisaidia timu ya taifa, Taifa Stars au timu ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars.

Wanaona kuwa kuwepo kwa wachezaji 12 wa kigeni, kunaua vipaji vya wachezaji wazawa.

Wapo wanaotaka wachezaji wa kigeni waendelee kuwa 12, waongezeke au kusiwe kabisa na idadi. Nao wana sababu zao. Wanasema idadi inayotamkwa 12 ya wachezaji wa kigeni haifikiwi na timu zote 16 zinachocheza Ligi Kuu. Timu ambazo zina uwezo huo sana sana ni Simba, Yanga, Azam na Singida Black Stars. Zilizobaki zinasajili wachache wachache na zipo ambazo hazina kabisa wachezaji wa kigeni. Hapo wanashangaa ni kwa nini wachezaji wachache tu wa kigeni wanaonekana wanawabana wazawa?

Binafsi naungana na hawa ambao hawaoni shida kuwa na idadi kubwa ya wageni kwenye ligi yetu.

Huwa najiuliza kama wachezaji wa kigeni wanazuia kuonekana kwa vipaji vya wazawa, basi wachezaji wazawa wa klabu za Simba na Yanga wasingeonekana kabisa na kuchaguliwa kwenye vikosi vyetu vya timu ya taifa. Nadhani wachezaji wa klabu ambazo hazisajili wachezaji wa kigeni ndizo zingekuwa na wachezaji wengi Stars. Kwa sababu hawabanwi. Wao wanacheza mechi zote 30 na vipaji vyao vinaonekana.

Nilitegemea klabu kama Mashujaa FC, JKT Tanzania na zingine chache zingekuwa na lundo la wachezaji Taifa Stars au Kilimanjaro Stars kwani hawabugudhiwi na mtu yoyote.

Nilikuwa majiuliza maswali mengi tu, nikasema ipo siku tutajua. Lilikuwa ni suala la muda tu.

Michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo imezishirikisha timu za taifa, imetuonyesha kuwa kwenye soka kinachotakiwa ni kipaji na kujituma, siyo kutengeneza kanuni, au kukataza mtu mwenye uwezo asicheze, ili kumsaidia mwenye uwezo mdogo.

Ni sawa na wazazi kijiji kukataza wanafunzi wenye uwezo mkubwa darasani wasifanye mtihani na watoto wao, wakihofia hawatofanya vyema, badala ya kufurahia kupima uwezo wao.

Timu ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars ilikuwa na wachezaji wengi kutoka klabu ambazo hazibanwi na wachezaji wa kigeni. Hii ilikuwa ndiyo njia ya kuwasuta wanaopenda wachezaji wa kigeni.

Tulitegemea kwa vile wachezaji wa Simba, Yanga na hata Azam hawapo kwenye kikosi cha Kilimanjaro Stars, wachezaji wa timu nyingine zilizobaki wangetumia fursa hiyo kuonyesha vipaji vyao na kuisaidia timu kwenye michuano ya mapinduzi, lakini imekuwa tofauti.

Katika michuano hiyo ya Mapinduzi, Kilimajaro Stars imejikuta ikipoteza mechi zake zote tatu ilizocheza na kuondolewa kwa aibu kwenye michuano hiyo.

Kilichoonekana kuna uzoefu fulani ulikosekana. Tuseme ukweli tu kuwa wachezaji wa Simba, Yanga na Azam wanapata changamoto kutoka kwa wachezaji wa kigeni ambao wanafanya wasibweteke, badala yake wanajituma na kufanya mazoezi kwa bidii ili kupigania namba.

Hilo haliwi faida kwao na klabu zao tu, bali hata kwa timu za taifa kama tulivyoona.



# Kijana amepotea, atakayemwona atoe taarifa

**Na Halfani Chusi**

NOEL Moisani, Mkazi wa Daima Soko Kiwalani jijini Dar es Salaam, amepotea tangu Januari Mosi, mwaka huu.

Akizungumzia kupotea kwake jana, baba yake mdogo, Stephens Ole Kipuyo, alisema siku hiyo, wakati anatoka nyumbani alikuwa amevaa fulana ya kujivu ya mikono mifupi iliyoandikwa 'UMOJA WA WANAUME KKKT YOMBO' na suruali ya rangi ya mistari ya kahawia na viatu vyeusi.

"Mwanangu huyo, nilimchukua Arusha kwa baba yake aje kusoma na alikuwa tayari ameshamaliza masomo yake na yeye ni kijana wa jamii ya kimasai lakini bahati mbaya hasikii na wala hawezi kuongea vizuri (bubu na kiziwi).

"Nilishatoa taarifa Kituo cha Polisi Buguruni na nikapewa RB namba 66/2025 ninaomba kwa yoyote atakayemwona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichokaribu yake au kupiga simu namba 0767683129 au 0784783129," alisema baba yake huyo.

# CHADEMA Singida wamkana mwenyekiti wao

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Singida Mjini, Swahibu Mohamed, amesema si kweli kwamba wajumbe wote 29 wa mkutano mkuu kutoka Mkoa wa Singida wanamuunga mkono mgombea uenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mohamed alisema kikao kilichoitishwa juzi Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Omari Toto, na kutoa tamko kwamba wajumbe wote 29 ambao ni wajumbe watakaopiga kura katika mkutano mkuu utaofanyika Januari 21, wanamuunga mkono Lissu si za kweli.

Kauli hiyo ya Mohamed imekuja siku moja tu baada ya Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa kutoa tamko kwamba mkoa unamuunga mkono Lissu.

"Mkutano tulioitiwa na Mwenyekiti wa Chadema Mkoa tuliambiwa ni wa mashauriano lakini kwa sababu akidi ya wajumbe haijatimia tumeshangaa mwenyekiti anaita waandishi wa habari na kutoa tamko kwamba CHADEMA Mkoa wa Singida wanamuunga mkono Lissu," alisema.

Mohamed alisema kwa mujibu wa katiba ya chama, wajumbe watakaopiga kura katika mkutano mkuu wa uchaguzi ni mwenyekiti, katibu na mjumbe wa mkutano mkuu kutoka kila jimbo ambao wanafanya jumla ya wajumbe 29 kutoka mkoa wa Singida.

Alisema mkutano huo uliofanyika juzi Singida mjini, wenyeviti na makatibu wa majimbo yaliyoko mkoa wa Singida hawakuwapo, hivyo linapotolewa tamko kwamba wajumbe wote wa Singida wanamuunga mkono Lissu si kweli.

Kwa mujibu wa Mohamed ambaye ni mlinzi wa Mbowe, kati ya wajumbe 29 wanaotoka Mkoa wa Singida ana uhakika wajumbe 20 wanamuunga mkono Freeman Mbowe.

Juzi, Toto akitoa tamko, alisema sababu zinazowafanya wamuunge mkono Lissu ni kutokana na suala la fedha za ruzuku zinazotolewa kwa chama.

Toto alisema CHADEMA kila mwezi kimekuwa kikilipwa Sh. milioni 107 kama ruzuku ya chama lakini katika hali ya kushangaza fedha hizo zimekuwa zikiishia makao makuu bila kupelekwa mkoani kwa ajili ya maendeleo ya chama.

"Fedha za ruzuku ambazo zinatolewa kwa ajili ya chama tunaimani Lissu akishakuwa Mwenyekiti mgawanyo utakuwa unakuja hadi huku mikoani kwa ajili ya shughuli za chama tofauti na sasa ambapo zinaishia makao makuu tu," alisema.

Alisema propaganga zinazoenezwa kwamba Lissu anaungwa mkono na wanachama ambao si wapigakura ni uongo na wanamdanganya Mbowe lakini kimsingi mfano katika mkoa wa Singida asilimia 75 Lissu anaungwa mkono.



Mwenyekiti mpya wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Hans Nkya (wa pili kulia), akizungumza wakati akiwashukuru wajumbe waliomchagua kwa kumpa kura zote 35 za ndiyo, katika uchaguzi uliofanyika juzi. **PICHA: GIFT**

# Mabilioni Korea kukuza uchumi Tanzania

**Na Benny Mwaipaja,**
DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Dola za Marekani bilioni 2.5 zilizoahidiwa na Korea Kusini kwa Tanzania hivi karibuni, zitasaidia kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo itakayochangia kusisimua ukuaji wa uchumi wa nchi na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Dk. Nchemba alisema hayo juzi alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania, Eunju Ahn. Pamoja na mambo mengine, walijadili namna ya kuimarisha zaidi ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kati ya nchi hizo mbili.

"Nchi yetu inasubiri kwa hamu kubwa utekelezaji wa miradi inayotokana na fedha hizo na hata katika hotuba yake ya mwisho wa mwaka 2024, Rais Samia Suluhu Hassan, alielezea kwa kina fedha hizo zitakavyotumika kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye lengo la kutimiza ajenda ya kitaifa ya kuwaletea Watanzania maendeleo," alisema.

Dk. Nchemba alisema makubaliano ya miradi itakayotumia fedha hizo iko katika sekta muhimu za maendeleo itakayochangia kukuza ajira, uchumi na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Waziri Nchemba aliahidi kuwa Tanzania iko tayari kuongeza kasi ya ushirikiano kati ya nchi hizo ili kufanikisha malengo ya uhusiano uliodumu kwa miaka mingi kati yake na Korea kwa faida ya wananchi wa pande hizo mbili.

Balozi Ahn kwa upande wake alisema Korea inaitazama Tanzania kama mdau wake mkubwa wa maendeleo na haijawahi kushuhudiwa nchi yoyote Afrika ikipewa fedha nyingi kiasi cha dola za Marekani bilioni 2.5 kwa wakati mmoja kama ilivyofanyika kwa Tanzania. Ahn alisema kupitia fedha hizo, Korea itaisaidia Tanzania kutekeleza miradi 12 ya kimkakati iliyowasilishwa na serikali, ambayo inatarajiwa kukuza uchumi wa nchi kupitia miradi mbalimbali itakayotekelezwa na serikali na sekta binafsi. Alisema Korea inaiona Tanzania kuwa nchi yenye maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii na kwamba muda mfupi ujao itafikia viwango vya juu vya ukuaji wa uchumi kutokana na umahiri wa usimamizi wa shughuli zake za kiuchumi ikilinganishwa na mataifa mengi ya kiafrika na ulimwengini kwa ujumla. Katika kikao chao, Dk. Nchemba na Balozi Ahn, walijadiliana kuhusu fedha hizo ambazo mkataba wake ulitiwa saini Juni 2, 2024 nchini Korea na kushuhudiwa na marais wa nchi hizo mbili.

Pia walijadiliana kuondoa changamoto ya utozaji kodi mara mbili na ukwepaji kodi kwa kampuni zinazowekeza katika nchi hizo mbili pamoja na kuvutia uwekezaji.

# Watu 14,000 wana matatizo macho Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI 14,624 waliopimwa magonjwa ya macho katika kipindi cha mwaka 2024 mkoani Shinyanga, wamebainika kuwa na matatizo makubwa ya ugonjwa wa macho, wengi wakiwa na mtoto wa jicho.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Huduma za Macho mkoani Shinyanga, Dk. Joseph Edward, alipozungumza na waandishi wa habari kutokana na utolewaji wa matibabu bure ya macho kwa wananchi mkoani hapa kutoka kwa madaktari bingwa wa macho wa Hospitali ya Dr Agarwals tawi la Mwanza.

Dk. Edward alisema takwimu hizo ni za miezi 10 iliyopita na kuwa kati ya wananchi hao 14,624 waliokutwa na matatizo hayo huku 1,213 wakiwa na tatizo la mtoto wa jicho na kwamba waliwafanyia upasuaji.

"Ujio huu wa madaktari bingwa wa macho hapa mkoani Shinyanga, utasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo ya macho kwa wananchi wa mkoa huo, ambalo linawasumbua sana," alisema.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga, Dk. Moshi Lyoba, alisema wananchi wengi wamejitokeza kupata matibabu hayo na kwamba kwa asubuhi tu ya jana waliandikisha wananchi zaidi ya 250, na kuonyesha kwamba tatizo la macho ni kubwa.

Daktari Bingwa wa Macho, Abubakari Mwatute, kutoka Hospitali ya Macho Dr. Agarwals Tawi la Mwanza, alisema kati ya wananchi 10 ambao wanawafanyia uchunguzi, saba hadi wanane wanakabiliwa na tatizo la mtoto wa jicho.

Mmoja wa wananchi waliopatiwa matibabu hayo, John Lucas, aliiomba serikali kuendelea kushirikiana na wadau wa afya na kuwapeleka madaktari bingwa wa macho ili wasaidiwe kupata matibabu bure.

Alisema asilimia kubwa wanashindwa kupata huduma hiyo kutokana na kutokuwa na uwezo wa kifedha kuwafuata katika hospitali za kibingwa.



Daktari Bingwa wa Macho kutoka Hospitali ya Macho Dk. Agawals, Tawi la Mwanza, Abubakari Mwatute (kulia), akifanya uchunguzi wa macho kwa mwananchi John Lucas, wakati wa zoezi la utoaji wa matibabu ya macho bure kwa wananchi wa Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bodaboda waandamana kisha kufunga barabara kisa kunyanyaswa na polisi

**Na Remmy Moka**

WAENDESHA pikipiki, maarufu 'bodaboda' pamoja na bajaji mkoani Kigoma wameandamana na kufunga barabara katika eneo la mzunguko kwa madai kwamba wamechoka kunyanyaswa na kukamatwa ovyo na Jeshi la Polisi mkoani humo.

Maandamano hayo yaliyofanyika juzi yaliingiliwa kati na kuzimwa na Jeshi la Polisi ambalo lilitumia silaha yakiwamo mabomu ya machozi huku baadhi ya madereva hao wakitiwa mbaroni kwa madai ya kusababisha vurugu hizo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa maandamano hayo, bodaboda hao akiwamo Chita Jackson, walisema wamekuwa wakifanya shughuli hizo bila uhuru licha ya wao kuwa sehemu ya upatikanaji wa pato la taifa.

Jackson alidai kuwa manyanyaso hayo ni pamoja na kukamatwa mara kwa mara bila sababu maalum licha ya kujitahidi kufuata sheria na taratibu wanazoelekezwa kwa ajili ya usalama barabarani.

Alisema kila wakikamatwa kwao wamekuwa wakitozwa faini hadi Sh. 100,000 ili kupata dhamana katika vituo vya polisi hali inayowafanya baadhi yao kushindwa kuendelea na kazi hiyo na kuingia katika hatihati ya kujiingiza katika makundi ya wezi.

Bodaboda mwingine, Hamis Abdullah, aliwashtumu askari wa usalama barabarani kuwakamata kwa vurugu na wakati mwingine kuwasababishia ajali huku wakiwatoza faini za kuanzia Sh.50,000 hadi 150,000 pale wanapokutwa na makaso mbalimbali yakiwamo kutovaa kofia ngumu.

Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda na Bajaji Mkoa wa Kigoma, Samwel Mtema, alisema hajapendezwa na hatua hiyo iliyofikiwa na madereva wenzake na kuwa tayari walikuwa wameanza kuongea suala hilo na viongozi wa kamati ya usalama barabarani mkoa.

> **"Serikali ilitangaza nauli halali Desemba mwaka 2023 na kuanza kutumika nchi nzima na mkoani Tabora tulimwambia Mkuu wa Mkoa ambaye aliwaita wadau...**

Alisema madhumuni ya kamati ya usalama mkoa kuja na operesheni iliyopo kwa sasa ni ni kukagua vyombo ambavyo havijakidhi vigezo pamoja na madereva wasiofuata sheria na taratibu.

Alisema operesheni hiyo inalenga kusaidia usalama wa waendesha bodaboda pamoja na watumiaji wengine wa barabara na vyombo hivyo hivyo kuwataka kutii sheria bila shuruti. Akizungumza katika eneo la tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Philemon Makungu, alisema baadhi ya bodaboda hawana leseni akitaja sababu kuu kuwa si raia wa Tanzania, hivyo hawana vitambulisho vya taifa (NIDA).

Kamanda Makungu alisema wametoa elimu kwao mara kwa mara kuhakikisha wanafuata sheria za barabarani bila mafanikio hivyo kuanzisha operesheni hiyo inayowalenga wale tu wasiofuata sheria ikiwamo kuvaa kofia ngumu, kuwa na leseni, bima za pikipiki pamoja na kufuata sheria za usalama barabarani.

Alisema wanazungumza na viongozi wao kwa kuwa malengo ya jeshi hilo ni kuhakikisha amani na utulivu katika Mkoa huo huku akiwataka wale wote wanao lituhumu jeshi hilo, ama maofisa wake kwa namna yoyote kuwasilisha tuhuma hizo pahala husika ili zipatiwe suluhu.

"Tuhuma ni tuhuma tu walete tuhuma zao zisikilizwe na kupatiwa suluhu na si kufanya vurugu na kuongea bila kuwa na suluhu," alisema Kamanda Makungu.

# TCRA yakoleza kampeni ya 'Ni Rahisi Sana' Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania TCRA imeendelea na kampeni yake ya 'Ni Rahisi Sana' msimu wa pili katika viwanja vya Nyamanzi Fumba Zanzibar.

Kampeni hiyo inafanyika katika maonesho ya kimataifa ya biashara kuelekea maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofunguliwa rasmi na Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, Januari 5, mwaka huu.

Msimu huu wa pili ulioanza rasmi Januari Mosi, mwaka huu, kampeni hiyo imejikita katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kikoa cha DOT TZ.

Maofisa walioko katika banda la TCRA, Sophia Mabada na Jasmine Kiyungi, walisema kutumia kikoa cha DOT TZ kutasaidia kumtambulisha mhusika au mfanyabiashara kama ni mzawa au mwenyeji wa Tanzania au biashara hiyo makao makuu yake yapo Tanzania moja kwa moja bila kutafuta taarifa nyingine.

"Suala hili litamwezesha mhusika kukubalika na kuaminiwa kwa urahisi, hivyo kufanikisha kufanya shughuli zake mbalimbali kwa urahisi," alisema Mabada. Kiyungi alisema kikoa cha DOT TZ kina umuhimu mkubwa kwa kuwa kinamhakikishia mtumiaji wa kikoa hicho ulinzi na usalama kwa kuwa kimesajiliwa Tanzania, hivyo taarifa na miundombinu yote ya kikoa hicho bado vitakuwa viko Tanzania. "Kwa hiyo hata kama kuna hitilafu yeyote kwa kuwa miundomninu yote ya kikoa cha DOT TZ iko Tanzania basi itakuwa ni rahisi kutatua, hivyo turudi nyumbani kwenye kikoa chetu," alisema.

Kampeni ya 'Ni Rahisi Sana' tangu kuanza Oktoba Mosi, 2024, imeleta matokeo makubwa kwa vijana, watoto, wazee na wadau wa mawasiliano.

Takwimu zinaonesha kuwa kampeni hiyo imesaidia watu mbalimbali kuepuka kadhia zinazopatikana wakiwa katika matumizi mbalimbali ya huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kama vile kutapeliwa mtandaoni na kwamba kumekuwa na mwitikio mkubwa wa kuripoti matukio ya uhalifu mtandaoni kupitia namba 15040.

Kampeni hiyo imesaidia kupunguza matumizi ya laini za simu zilizokuwa zimesajiliwa na matumizi halali kutokana na hamasa ya kuhakiki namba zilizosajiliwa na kitambulisho cha NIDA kupitia namba *106#.

Kwa kuhakiki huko kulisababisha watu waliogundua kuwa vitambulisho vyao vimesajili laini za simu wasizozitumia kwa matumizi halali waliweza kuwasiliana na watoa huduma wao na kuomba kufutwa kwa namba hizo. Meneja wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Esuvatie Masinga, alisema pamoja na kuendelea na msimu huu wa pili wa kampeni ya 'Ni Rahisi Sana', bado hawataacha kuelimisha umma kuhusu fursa muhimu zinazopatikana katika huduma za mawasiliano.

Masinga alisisitiza kuwa jamii inapaswa ichangamkie fursa zinazopatikana kwenye huduma za mawasiliano kama vile ajira na biashara kwa kutangaza biashara hizo mitandaoni na hivyo kujipatia kipato na kukuza uchumi wao. Alisema dunia kwa sasa imefika mabadiliko makubwa na kila kitu kwa sasa kinaendeshwa kidigitali, hivyo wataendelea kuelimisha watu hasa watoto wadogo na wabunifu mbalimbali kuanza kuitambua na kuipenda teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili wanapokuwa wawe wameshapata uzoefu mkubwa na ujuzi mkubwa wa kuitumia teknolojia hiyo katika kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii.





# Wenyeviti wa mitaa, vijiji wapewa somo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WENYEVITI wapya wa mitaa na vijiji katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, wametakiwa kuimarisha uhusiano baina yao, wananchi na wataalamu ili kuleta ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa wenyeviti hao yenye lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema wenyeviti ndio wenye kusimamia kundi kubwa la wananchi, hivyo kuwataka kuwaelewa na kuwachukulia kila mmoja kwa namna alivyo bila kumwacha mtu nyuma.

" Uongozi wenu umepewa dhamana ya kusimamia na kuongoza kundi kubwa la watu, hivyo wachukulieni kila mmoja kwa namna walivyo bila kuwaacha nyuma, vichaa ni wenu, walevi ni wenu, mashehe na mapadre ni wenu," alisema.

Aidha, Kiaratu aliwataka viongozi hao kushirikiana na kamati mbalimbali katika mtaa au kijiji anachokiongoza lengo likiwa ni kufikia malengo kimaendeleo.

"Shirikisheni kamati zilizopo eneo lako na hasa wataaalamu. Usijione kuwa ni mwenyekiti ukafanya maamuzi yasiyo shirikishi," alisema.

Pia aliwaagiza wenyeviti hao kusimamia vyema suala na ukusanyaji mapato na kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi zinawekwa wazi kwa wananchi. Amesisitiza pia suala la kusimamia uhifadhi wa mazingira kwa kuhimiza upandaji miti katika kaya na taasisi katika mitaa na vijiji vyao.

Kiaratu aliahidi kama halmashauri kutoa ushirikiano wa kina pale inapobidi kufanya hivyo kwa ajili ya maendeleo ya Manispaa ya Singida.

Wenyeviti 72 wa mitaa na vijiji waliochaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 2024, wamepatiwa mafunzo hayo yaliyotolewa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

# Bashungwa azindua mikakati sita ya mawasiliano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa, amezindua mikakati sita ya mawasiliano ya wizara na vyombo vyake vya usalama yenye lengo la kuimarisha mawasiliano kati ya serikali na jamii.

Pia amewataka wakuu wa vyombo vyote vya usalama nchini kuanza utekelezaji wa mikakati hiyo mara moja ili kutoa fursa kwa wananchi kupata taarifa za shughuli mbalimbali zinazofanya na serikali yao.

Bashungwa alibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mikakati hiyo iliyofanyika kwenye ukumbi wa Jeshi la Magereza Makao Makuu, Msalato jijini hapa.

Alisema mikakati hiyo iliyozinduliwa ni kwa ajili ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

"Ikumbukwe kuwa kuandaliwa kwa mikakati hii ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kuzitaka wizara na vyombo vya usalama kuwa na mikakati ya mawasiliano. Lengo kubwa ni kuimarisha mawasiliano kati ya serikali na jamii tunayoihudumia," alisema Bashungwa.

> **"Nimepitia mikakati hii na kujionea shughuli mbalimbali za kihabari zilizopangwa kufanyika, utekelezaji wa mikakati hii kwa weledi utasaidia kuimarisha suala zima la habari ...**

Alisema kuandaliwa kwa mikakati hiyo na kuzinduliwa kuwe chachu kwa Wizara na Vyombo vyake vya Usalama, kuhakikisha kuwa utekelezaji unaanza rasmi, kuanzia sasa na utekelezaji wake unafanyika kwa ufanisi.

"Nimepitia mikakati hii na kujionea shughuli mbalimbali za kihabari zilizopangwa kufanyika, utekelezaji wa mikakati hii kwa weledi utasaidia kuimarisha suala zima la habari na mawasiliano kwa umma.

"Miongoni mwa malengo ya kuandaliwa kwa mikakati hii ya mawasiliano ni kuongeza uelewa na ushiriki wa jamii katika masuala ya usalama wa raia na mali zao sambamba na utunzaji wa amani na utulivu wa nchi yetu," alisisitiza Bashungwa.

Pia aliagiza vitengo vya habari kwenye vyombo vya usalama, vinatengewa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati hiyo ya mawasiliano.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, alisema lengo la mikakati hiyo ni kuongeza uelewa, na ushiriki wa jamii katika masuala ya usalama wa raia na mali zao, sambamba na utunzaji wa amani na utulivu wa nchi.

Hata hivyo, alisema mikakati hiyo itatekelezwa kwa muda wa miaka miwili na baada ya hapo itafanyika tathimini ambayo itasaidia kubaini mapungufu yaliyopo na kuyafanyia kazi.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini (PDPC), Emmanuel Mkilia (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, akizitaka taasisi zote za umma na binafsi zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi kujisajili kabla ya mwezi Aprili mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkurugenzi ataka kasi tiba afya akili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, ameagiza Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe kuongeza kasi ya utoaji huduma za utengamao na afya ya akili kwa wananchi wenye uhitaji ili kuifikia idadi kubwa.

Dk. Ubuguyu alitoa wito huo jana jijini hapa alipofanya ziara ya kuangalia hali ya utoaji huduma katika hospitali hiyo na kujiridhisha na utoaji wa matibabu wakati huu ambapo serikali unataka kuifanya Mirembe kuwa taasisi inayojitegemea.

Alisema jamii ikipata elimu sahihi juu ya huduma za utengamao na afya ya akili itasaidia kuongeza uelewa wa utengamao na afya ya akili na kufanya wananchi kuhudhuria kliniki kwa wakati ili kupata matibabu sahihi. "Jamii ina uhitaji mkubwa sana wa huduma hizi za utengamao na afya ya akili hivyo kuna haja ya kuongeza kasi ya utoaji wa elimu juu ya huduma hizi na kuwafikia wananchi kwa wingi ili waweze kupata huduma sahihi kwa wakati na ubora unaohitajika", alisema. Dk. Ubuguyu pia alisema Mirembe imepiga hatua kubwa sana katika kuboresha huduma zake na kuhudumia wananchi japo tatizo la afya ya akili ni kubwa katika jamii hivyo kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya magonjwa yasiyoyakuambukiza.

Naye Mtaalamu wa Huduma za Utengamao na Tiba Mazoezi, Ally Shabani, kutoka Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe, aliomba kuongezewa vifaa tiba ili kuongeza kasi na ubora wa utoaji huduma ya utengamao na afya ya akili kwa wananchi wanaofika hospitalini hapo.





# 'Vivutio Zanzibar uthibitisho wa umaarufu uliopo'

**Na Mwnadishi Wetu**

KAIMU Mkurugenzi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Ofisi ya Zanzibar, Balozi Silima Kombo Haji, amesema ujio wa wajumbe wa nchi mbalimbali kutaka kuwekeza nchini unathibitisha umaarufu wa Zanzibar ulimwenguni.

Akizungumza na Sheikh el Amin Omer el Amin kutoka Sudan aliyefika ofisini kwake Maisara mjini Zanzibar kujitambulisha, alitumia fursa hiyo kumkaribisha kutembelea maeneo mbalimbali ya Zanzibar kujionea fursa za uwekezaji katika kisiwa hicho.

Balozi Kombo alimweleza Sheikh El Amin kuwa kwa sasa vipaumbele vya uwekezaji ndani ya Zanzibar ni biashara ya utalii, viwanda na uchumi wa buluu na kumshauri kufika Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ili kupata maelezo zaidi ya maeneo yaliyo tayari kuwekezwa.

Alisema uchumi wa buluu umekusanya masuala ya uvuvi wa bahari kuu, utalii wa bahari kupitia visiwa vidogo vidogo, mafuta na gesi, pamoja na usafirishaji wa baharini.

"Watanzania na Wasudani ni ndugu na wana uhusiano wa muda mrefu hivyo kuja kuwekeza katika Kisiwa cha Zanzibar kutaimarisha zaidi undugu wao," alisema Balozi Silima.

Naye Sheikh El Amin alisema ni mara ya kwanza kufika Zanzibar lakini amevutiwa na wananchi wake kutokana na ukarimu na ustaarabu waliyonao hasa kwa wageni wanaoingia nchini.

Alisema kabla ya kufika Zanzibar, alisikia sifa mbalimbali zinazotajwa kuwepo na kuzithibitisha baada ya kutembelea ambapo kwa sasa anatamani kuwa sehemu ya Zanzibar.

Sheikh El Amin alisema Zanzibar ina vivutio vingi na maeneo mbalimbali ya uwekezaji na kusema kuwa yupo tayari kuwekeza katika maeneo ya utalii Ili kukamilisha dhamira yake ya kuwa sehemu ya Zanzibar.

Sheikh El Amin ni mmoja wa Wasudan wanaoishi nchini Uingereza aliyefika Zanzibar kwa ajili ya kutafuta maeneo ya uwekezaji kupitia sekta ya utalii visiwani hapa.

# Waziri asifu ubunifu vikosi vya SMZ

**Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, amesema ubunifu wa vikosi vya SMZ kujiendeleza katika kuimarisha miradi yao ni moja ya mafanikio ya vikosi hivyo.

Waziri Rahma alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la kituo cha kuuzia mafuta makao makuu ya kikosi cha valantia (KVZ) Mtoni, Zanzibar.

Alisema ni faraja kuona kikosi hicho kikimiliki kituo cha kuuzia mafuta na ni biashara nzuri ambayo itaongeza kipato.

Waziri alisema ujenzi wa miradi hiyo ya uzalishaji mali, azma yake ni kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuongeza kiwango cha mapato kikosini kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli zao.

Alisema kituo hicho cha mafuta ni kielelezo cha uwezo na dhamira ya dhati ya maofisa na askari wa kikosi cha Valantia Zanzibar katika kuchangia maendeleo ya nchi.

"Nikupongezeni sana baada ya kusikia kuwa kituo hiki cha mafuta kimejengwa na mafundi wenyewe wa kikosi cha Valantia kwa kushirikiana na mzabuni ambaye anahusika katika ujenzi wa baadhi ya maeneo yanayohitaji utaalamu zaidi hadi kukamilika kwa mradi," alisema.

Pia alisema hatua hiyo inazidi kujenga imani kwa viongozi kuwa taasisi za kiulinzi ndio za kutegemewa katika kufanikisha shughuli za kimaendeleo sambamba na kudumisha amani ya nchi.

> **"Nikupongezeni sana baada ya kusikia kuwa kituo hiki cha mafuta kimejengwa na mafundi wenyewe wa kikosi cha Valantia kwa kushirikiana na mzabuni ambaye anahusika...**

"Kwa jinsi nilivyokagua kituo hiki na maelezo niliyopatiwa naridhika kwamba jengo hili limekidhi vigezo vilivyokubalika na kwamba itasaidia katika kutoa huduma za utoaji wa mafuta pamoja na huduma zingine za kibiashara kwa wapiganaji wetu lakini pia kwa wananchi wote wa Zanzibar watakaohitaji huduma zilizoainishwa kwenye taarifa ya kitaalamu," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Idara Maalum, Serikali za Mitaa na Vikosi vya SMZ, Issa Mahfoudh Haji, alisema ujenzi wa kituo hicho umegharimu Sh. bilioni 195 hadi kukamilika. Alisema inatia faraja kuona vikosi vya SMZ kuwa na miradi ya kibiashara ya kuwaongezea kipato kwa manufaa ya kikosi husika ili kuondokana na changamoto ndogo za upatikanaji wa fedha ndani ya kikosi hicho.

Kamanda Mkuu wa Kikosi hicho, Meja Said Ali Shamuhuna, alisema kukamilika kwa kituo hicho ni faraja kwa wananchi wa Zanzibar kupata huduma ya mafuta kwa saa 24, hivyo aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana katika kuendeleza mradi huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi, Machano Othman Said, alisema vikosi vya idara maalum vya SMZ vimebadikika katika utendaji wa kazi na sasa ni wabunifu zaidi kuanzisha miradi ya maendeleo kuviongezea kipato.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi wa Ujenzi wa Shirika la Nyumba, Juma Saleh Juma (kushoto), kabla ya kufungua nyumba za makazi ni biashara Mnadani Darajani, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, jana. **PICHA: MAELEZO ZANZIBAR**

# Wazazi wakumbushwa umuhimu elimu kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wazazi na walimu wana jukumu muhimu la kuwasimamia watoto kusoma kwa bidii baada ya serikali kuandaa mazingira mazuri ya kusomea.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo alipozindua shule mpya ya ya Ghorofa ya Msingi ya Kojani , Wilaya Ndogo ya Kojani, mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema ujenzi wa shule unaofanywa na serikali lengo lake ni kuhakikisha wanafunzi wanapata fursa nzuri ya kupata elimu katika mazingira bora.

Dk Mwinyi alisema amefarajika na kazi nzuri ya usimamizi wa shule hiyo ya Kojani uliofanywa na watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wakala wa Majengo pamoja na mkandarasi kwa kumaliza ujenzi huo kwa wakati na kwa viwango bora.

Kuhusu ajira, aliagiza wizara za afya, elimu na utumishi kuhakikisha zinapofanyika hususan Kojani, ni lazima wapewe vijana wa kisiwa hicho na kuzitaka taasisi hizo kutekeleza hilo.

Agizo lingine alilitoa kwa Wizara ya Afya ni kupeleka boti moja ya matibabu (ambulance ya baharini) katika kisiwa hicho ili kurahisisha huduma za wagonjwa ambao watapewa rufani.

Pia alisema hatua hiyo itarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi wa Kojani na kuahidi kuwa serikali itaongeza wafanyakazi Kojani ili huduma ndogo katika nyanja mbalimbali zitolewe kisiwani humo.

Akizungumzia mabadiliko ya tabianchi na tatizo la maji ya bahari kuingia katika makazi ya watu, Dk. Mwinyi aliahidi kuwa serikali itakaa na wataalamu kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Mke wa Rais wa Dk. Mwinyi, Mama Maryam Mwinyi, aliwataka wadau wa maendeleo kuunga mkono juhudi za kumaliza changamoto wanazokabiliana nazo watoto wa kike wakiwa shuleni.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema ujenzi wa Shule hiyo umegharimu Sh. bilioni 5.382 ikiwa na madarasa 32, maabara, chumba cha kompyuta, maktaba na ukumbi wa kufanyia mitihani na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,305 kwa mkondo mmoja.







# GIGY MONEY KAAMUA

MWANAMUZIKI mwenye utata, Gigy Money, amesema yuko tayari kukutana na viongozi wa dini kwa ajili ya kumuhubiria neno la Mungu ambalo litamtoa katika maisha ya majaribu.

Gigy Money, amesema anamshukuru msanii mwenzake Irene Uwoya, ambaye kwa sasa ameanzisha kanisa kwa juhudi zake za kumtaka kumjua Mungu.

Hivi karibuni Uwoya na Gigy Money walikuta na kufanya mazungumzo ambayo yanaaminika yakuwa ya kumshawishi kuacha mambo yasiyofaa na kumrudia Mungu.

"Niko tayari kumtumikia Mungu, lakini sio utayari wa kuwa mchungaji. Mungu akimbiwi, amekupa nguvu na akili ili kumtumikia yeye na katika maisha yangu ni suala la muda tu kila kitu kina muda wake," amesema Gigy Money.

Amesema kabla ya kufanya maamuzi sahihi ni lazima abadilishe mtindo wake wa maisha kutokana na ukweli kwamba Mungu anapenda mtu safi.

"Itabidi niwe msafi ili nimtumikie Mungu, naweza kubadilika na inawezekana kwa kila kitu kama Mungu amekuchagua," ameongeza.

Hata hivyo, amewaomba watu mbalimbali na viongozi wa dini kumuhubiria maneno ya vitabu ili kumfanya amjue Mungu ipasavyo na hatimaye kuachana na maisha aliyonayo sasa.

## BASI SAWA

### Appy ajipa tumaini



Mwanamuziki anayekuja kwa kasi katika Bongo Fleva, Appy, amesema kutoa wimbo na kuwa maarufu ni mapenzi ya Mungu na kwamba hakuna anayejua matokeo yanayokuja.

Akizungumza hivi karibuni mwimbaji huyo wa 'Watu Feki' amesema baada ya kufanya vizuri na wimbo huo, kinachompa wakati mgumu kutoa kibao kingine kitakachokuwa na ugumu zaidi.

"Naangalia namna ya kuandaa wimbo mwingine ambao utapendwa zaidi, hiyo ndio ninachofikiria kwa sasa kwani nina deni kubwa kwa mashabiki zangu ambao wanataka nyimbo nzuri na zenye ubora, amesema Appy.

### Amina Vikoba ungefanyaje kama usingepewa talaka?



MWIGIZAJI maarufu Amina Ahmed maarufu kama Amina Vikoba, amesema ameamua kudai talaka baada ya kuona kama angeendelea kubaki katika ndoa yake yangemkuta mambo mazito.

Amina ambaye amepata umaarufu kupitia tamthilia ya Kombolela, ameeleza kwamba ndoa yake na mume wake ilivunjika siku nyingi kutokana na vitendo alivyofanyiwa, hivyo Mahakama ilipoamua kuvunja ndoa hiyo moyo wake ulijaa furaha.

"Nilipopata talaka tu tuliamua kuweka mtandaoni ili kila mtu ajue kwa sasa niko singo ili kuonyesha furaha yangu. Nisingeweza kuendelea na ndoa ile kwa sababu kila kitu kilishindikana na kama ningevumilia mambo yangekuwa mazito," amesema Amina Vikoba.



## MARIOO JIFUNZE KIINGEREZA

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Marioo amesema pamoja kuwa yeye ni CEO wa lebo ya Badnation, lakini hajui kirefu cha neno hilo kwa lugha ya Kiingereza.

Marioo kupitia lebo yake hiyo ameanza kutoa wasanii wakali na alipoulizwa kama anajua kirefu cha neno hilo, alisema yeye anatambua kuwa ni nafasi ya juu katika taasisi, lakini kirefu chake hafahamu.

Ahh...mimi sijui kirefu chake lakini naamini ni kiongozi. Mimi ndiye CEO, lakini ukweli sijui kirefu chake maana sijasoma mimi sasa nitajuaje, alihoji baada ya kuulizwa kama anajua kirefu cha kifupi cha maneno hayo.

## FILAMU

# Kala kuku na mayai yake

**Na Adam Fungamwango**

NI tabia iliyojengeka kwa baadhi ya wanaume kuwatia mimba wasichana na kuwakimbia.

Leo tutaiangalia filamu ya 'Mume Aliyekimbia', ambayo inaelezea kisa cha kusikitisha kilichotokana na kosa la mtu mmoja ambaye anakuja kufanya kosa lingine kwa mara ya pili linaloleta matatizo kwenye familia yake na yeye mwenyewe.

Imechezwa na Suleiman Barafu, Stanley Msungu, Riyama Ally, Najma Ally na Catty Rupia na wengineo. Inaanza kuonyesha kuwa Barafu anaishi vema na mkewe Catty.

Shetani anamwingia na kuingia kwenye penzi na msichana mwanafunzi wa sekondari aitwaye Najma. Penzi linanoga kiasi cha mkewe kujua kuwa mumewe ana matatizo kwa sababu alibadilika tabia.

Riyama ambaye ni mama wa Najma kutokana na kuletewa pesa na binti yake akawa hajui binti yake aendelee na masomo au aendelee na mchezo wake mchafu. Najma anapata mimba. Inamchanganya mama na Barafu mwenyewe.

Najma kuitoa hataki na Barafu ana mke. Binti anajiona bora azae ili awe mke wa Barafu.

Barafu anaandaa mbinu kabambe na rafiki yake Msungu. Mbinu yenyewe ni kumuua Najma. Kwa sababu amekataa kutoa mimba na yeye ni mwanafunzi kitu ambacho kilimtisha Barafu kuwa anakaribia kuingia kwenye mdomo wa jela.

Msungu anamuua Najma, lakini anakamatwa alipokuwa anakwenda kutupa maiti iliyokuwa ndani ya gari.

Hata hivyo anasema kuwa yeye si mhusika ila alitumwa. Anaachiwa kwa sharti moja tu la kumkamatisha mhusika.

Barafu katika pitapita yake anakutana laivu na Riyama, mama yake marehemu Najma. Wanakumbukana. Miaka mingi iliyopita kwenye kijiji kimoja, alimpachika mimba Riyama na kukimbia. Alijifungua mtoto wa kike akamwita Najma. Kumbe Barafu alimpa mimba binti yake. Lakini pia alifanya njama ya kumuua.

Polisi na Msungu wanakwenda kumchukua Riyama, wakimweleza kuwa wamempata muuaji wa binti yake. Wanakwenda nyumbani kwa Barafu na kumkamata. Riyama alipoona sura ya Barafu na kujua kuwa yule ndiye alimpa mimba binti yake na pia kumuua anaanguka chini na kuzirai.







## Simple Boy usikate tamaa

RAPA kutoka Kenya, Stevo Simple Boy, amesema safari yake ya kuja Tanzania wiki moja iliyopita kwa ajili ya kukutana na Harmonize kupanga namna ya kufanya kolabo.

Amesema kwamba alihisi Harmonize alivutiwa na ngoma yake mpya 'Inauma lakini itabidi umezoea' aliyoifanya miaka ya nyumba baada ya kumuona bosi huyo wa lebo ya Konde Music Worldwide akiimba kipande chake.

"Tanzania nilikuwa nimeenda kumtafuta Harmonize na Diamond Platnumz, kwa bahati mbaya sikukutana nao kwa sababu ya muda. Lengo langu lilikuwa kama naweza kurudi nyuma kidogo, kuna wakati ile ngoma yangu 'inauma lakini itabidi tuzoee' Harmonize aliimba,@ amesema.

# MWAKA MPYA NA MAMBO MAPYA

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni mwaka mpya na bado mbichi kabisa wa 2025. Wasanii hao hawakuwa nyuma. Baadhi yao walihakikisha ukiingia tu, basi watakuwa wanafyatua vibao na wao kuuanza kwa neema.

Leo tutawaangalia wasanii wa bongo fleva ambao ni kama waliingia studio na kurekodi ngoma zao, na wakawa wanasubiria mwaka mpya ili wazitoe kwenye kabati.

**Kusah - Blessings**

Kusah yeye wala hakusubiri. Januari Mosi, yaani mwaka mpya tu, akaamua kutoa ngoma yake iliyokuwa kabatini. Inaitwa 'Blessings', ni moja kati ya ngoma za mwanzo kabisa za bongo fleva mwaka huu.

**B2K- Neno hili**

Siku hiyo hiyo ya mwaka kuna msanii naitwa B2K, alifyatua ngoma yake aliyoiita 'Neno Hili'.

Hii ameichukua kwenye vibonzo ambavyo kwa sasa vinashika chati sana hapa nchini. Ndani ya vibonzo hvyo kuwa neno linalotajwa 'neno hili siyo geni hapa mjini.'

**D Voice-No**

Ngoma hii imetoka Januari 3, siku tatu tu baada ya mwaka mpya. D Voice aliona isiwe tabu. Baada ya mwaka kupinduka, anasubiri siku zake tatu, akaamua kuipua ngoma hii, ambayo hadi inaandikwa hapa ilikuwa nafasi ya nane kwa 'kutrendi' kwenye mitandao ya kijamii.

**Marioo feat Bien - Nairobi**

Marioo, ni moja kati ya wasanii wa mwanzo mwaka huu kutoa ngoma. Akishirikisha Bien, ametoa wimbo wake aliouita 'Nairobi',

Aliutoa Januari 6 mwaka huu, na umeshika nafasi ya 16 kwa 'kutrendi' kwenye mitandao ya kijamii hadi hivi sasa.

**Mbosso-Kupenda**

Hivi ninavyokwambia ni kwamba, msanii Mboso, yupo mbioni naye kutoa ngoma iiitwayo 'Kupenda', siku chache zijazo tu.

Tayari ameshaweka 'clip' yake fupi kwenye mtandao wake wa kijamii iliyoonyesha amemaliza maandalizi yote na kilichobaki kuitoa kabatini tu.



# Chloe asifia ya Burna Boy



MWANAMUZIKI nyota wa Marekani, Chloe Elizabeth Bailey, hatimaye amezima uvumi kuhusu uhusiano wake na msanii nyota wa Nigeria, Burna Boy.

Mwimbaji huyo mzaliwa wa Atlanta, amesema alikuwa na wakati mzuri alipokutana na Burna Boy wakati waliposhiriki pamoja katika tamasha la Detty Desemba lililofanyika katika jiji la Lagos.

"Nigeria ni nzuri sana. Nilikuwa na wakati mzuri zaidi. Nilikula chakula kizuri, nilikula supu ya pilipili na kuku wengi wa viungo. Ni nzuri sana. Kwa kweli nilikuwa na wakati mzuri," amesema.



## Spyro ukiwapa usiwasimange

MKALI wa muziki wa Nigeria, Oludipe Oluwasanmi David, maarufu kama Spyro, amesema amechoshwa na kitendo cha kutoa pesa kwa watu wanaomuomba mara kwa mara.

Mwanamuziki huyo wa pop alibainisha kuwa yeye hutumia wastani wa naira 100,000 kila siku kwa ajili ya kutoa kama msaada kwa watu wa aina hiyo.

Amesema kwa sasa imekuwa shida kwake kwani kila wakati anatarajia kupata maombi kutoka kwa watu mbalimbali wakiamini yeye ni mtu maarufu.


## Jlo, Affleck wakubaliana

WANANDOA mastaa Ben Affleck na Jennifer Lopez, wamefikia makubaliano ya mchakato wa kupeana talaka kwa amani ifikapo Febtuari 20.

Nyaraka za kisheria za mchakato huo zilionyesha kuwa wawili hao wamekubaliana masharti ambayo yatanufaisha pande zote mbili.

Katika makubaliano hayo, wote wawili Jennifer Lopez na Ben Affleck watahifadhi mapato waliyopata binafsi wakati wanaishi kama mume na mke.

Pia hakuna mtu ambaye atalazimika kutoa msaada kwa yeyote kama fidia.





## Mwaka wao waache watambe

WAIGIZAJI maarufu kutoka Hollywood, Zendaya na Tom Holland, ambao kwa sasa wamekuwa gumzo baada ya kuwa wapenzi, imeelezwa wawili hao walichumbiana wakati wakiwa likizo.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ, Holland ambaye ni nyota katika filamu za Spider-Man na Zendaya walivishana peke katika moja ya nyumba za familia ya Zendaya nchini Marekani.

Hata hivyo, vyanzo kutoka familia za wawili hao zinaeleza wazazi wao hawakuwepo wakati wanatekeleza jukumu hilo muhimu katika maisha yao.

## Darlington ulikotoka katoe sadaka

MAHAKAMA ya Shirikisho nchini Nigeria, imetoa amri ya kuachiwa kwa msanii wa muziki, Speed Darlington, baada ya kukaa mahabusu kwa mwezi mmoja.

Hakimu wa mahakama hiyo aliamuru Inspekta Mkuu wa Jeshi la Polisi la Nigeria, kumshtaki mwanamuziki huyo ndani ya saa 48 au kumwachilia huru bila masharti.

Uamuzi huu mpya unakuja wiki mbili baada ya mwimbaji huyo mwenye utata kupewa dhamana na mahakama, lakini aliendelea kubaki mahabusu bila maelezo yoyote kutoka jeshi la polisi.





# Afariki dunia madai ya kunywa pombe za kienyeji kupita kiasi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Mtaa wa Sawe, Kata ya Maisaka katika Halmashauri ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, Yona Angres, amepoteza maisha, baada ya kudaiwa kunywa pombe nyingi za kienyeji kupita kiasi.

Jana, Kamanda wa Polisi wa mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Ahmed Makarani, alisema Angres alifariki dunia kwa kuzidiwa na kiwango cha kilevi kinachotokana na pombe kali za kienyeji, ambazo hazina uthibitisho wa kisayansi. Aisema polisi wanaendelea na uchunguzi juu ya kifo hicho.

Alipotafutwa kuzungumzia matumizi ya vilevi kwenye eneo lake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Sawe, John Paul, alisema Angres alifariki dunia baada ya kunywa pombe nyingi za kienyeji zinazotengenezwa holela katika mji huo. "Baadhi ya watu waliokuwa naye kwenye eneo hilo, walisema huyo jamaa (Angres) alikunywa pombe nyingi za kienyeji na kufariki dunia baada ya muda mfupi," alisema Paul. Mmoja wa mashuhuda, Isack Dere, alisema Angres alianza kunywa pombe hizo tangu asubuhi na ilipofika jioni, ndipo alipozidiwa na kupoteza maisha.

**"Baadhi ya watu waliokuwa naye kwenye eneo hilo, walisema huyo jamaa (Angres) alikunywa pombe nyingi za kienyeji na kufariki dunia baada ya muda mfupi," alisema Paul.**

Kutokana na tukio hilo, alitaka jamii ya eneo hilo kunywa pombe zilizothibitishwa na mamlaka na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na kupata alama ya ubora na kupata uthibitisho wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuliko kunywa pombe zilizotengenezwa holela. "Hapa Babati kuna kiwanda kizuri cha vinywaji changamfu ambacho kina uthibitisho wa ubora wa viwango. Sasa kwa nini mtu unakunywa mataputapu hadi ufariki dunia kabla ya muda wako?" alihoji Dere.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Asia Juma, alisema Angres ni kijana aliyekuwa anafanya vibarua mbalimbali ikiwemo kusomba maji na kulipwa fedha. "Nadhani siku hiyo hakula chakula kisha akashiba ndiyo sababu akafariki dunia kwa kunywa pombe nyingi za kienyeji kupita kiasi," alisema Asia.



Baadhi ya wadau wa maendeleo wa Wilaya ya Babati Mjini, mkoani Manyara, wakiangalia kokoto zilizotolewa msaada na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM ya wilaya hiyo, Emmanuel Khambay (hayupo pichani), kwa ajili ya ujenzi wa choo cha Shule ya Msingi Kwaang'w, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wakumbushwa kulipa madeni MSD

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Jairy Khanga, ameshauri vituo vya kutolea huduma za afya nchini, vinavyodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kulipa madeni yote ili kuiwezesha kumudu ununuzi wa dawa na vifaa tiba nje ya nchi.

Dk. Khanga alishauri hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao kazi cha wadau wa MSD, Kanda ya Kilimanjaro.

Alisema wazalishaji wakuu wa bidhaa za afya wanatoka nje ya nchi, hivyo ni lazima MSD kujengewa uwezo wa kumudu ununuzi wa bidhaa hizo.

"Vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinavyodaiwa na MSD vizuri wahakikishe wanalipa madeni yao yote ili kuendelea kuipa nguvu MSD ya kununua dawa na vifaa tiba nje ya nchi ambako wanazalisha bidhaa hizo," alisema.

Alisema wazalishaji wengi wa bidhaa hizo za afya, wanatoka India, China hata Ulaya na havipatikani bure na zaidi ya asilimia 80 vinapatikana nje ya nchi.

Pia alisema kikao hicho kimeitishwa na MSD kwa lengo la kukutana na wadau mbalimbali ambao wanashirikiana na MSD ili kujadili mazuri na dosari zilizopo ili zifanyiwe kazi na kutoa huduma bora za afya nchini.

"Baadhi ya kazi kubwa za MSD ni kufanya manunuzi ya dawa kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma nchini. Lakini pia kufanya usambazaji wa vifaa vya afya mpaka ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya na kuhakikisha dawa zinatunzwa," alisema.

Aliipongeza serikali kwa kuisaidia MSD kuanza kujihusisha na uzalishaji wa vifaa tiba vya afya, kwani inasaidia upatikanaji wa dawa na baadhi ya vifaa tiba nchini.

Vilevile alisema upatikanaji wa vifaa vya afya kwa ajili ya Mkoa wa Kilimanjaro, upo asilimia 96 na baadhi ya halmashauri asilimia 98 sababu ya kazi nzuri za MSD na kazi nzuri ya serikali kwa kuongeza kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya za mkoa huo.

"Mkoa wa Kilimanjaro pekee kwa mwaka bajeti yetu ya dawa shilingi bilioni 12, hiki kiasi kikubwa hakijapata kutokea katika kipindi chote cha nyuma tangu nchi ipate uhuru, Mkoa wa Kilimanjaro kwa kipindi cha miaka miwili pia tumepata fedha zaidi ya Sh. bilioni 9.6 kwa ajili ya vifaa tiba," alisema.

Pia alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, hospitali na zahanati na fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kununulia vifaa tiba na kuwekwa kwenye vituo vipya vilivyojengwa katika mkoa huo.

Mkurugenzi wa Ugavi na Uendeshaji wa MSD, Victor Sungusia, alisema lengo la kukutana na wadau wanaohudumia masuala ya afya, ni kutathmini kiwango cha huduma wanazotoa na kusikiliza mapungufu yaliopo, ili wakayafanyie kazi na kuboresha kwa manufaa ya wananchi kupata huduma bora kama serikali inavyokusudia.

# UDP, Demokrasia Makini watoa neno uchaguzi CHADEMA

**Na Oscar Assenga,** TANGA

VYAMA vya siasa vya UDP na Demokrasia Makini, vimetoa mitazamo yao kuhusu wagombea wawili wa nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), huku vikitangaza hadharani vinamuunga mkono, Makamu Mwenyekiti wa sasa wa chama hicho, Tundu Lissu.

Uchaguzi wa viongozi wa juu wa CHADEMA, unatarajiwa kufanyika Januari 21 mwaka huu.

Akizungumzia uchaguzi huo jana jijini Tanga, Katibu wa Chama cha UDP Wilaya ya Tanga, Hemed Said, alisema kwa mtazamo wake, Lissu anafaa kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA taifa kutokana na uungwaji mkono kwa asilimia kubwa na chama chake.

Alisema mbali ya tofauti zao za mrengo wa kivyama, lakini wanamuunga mkono Lissu awe Mwenyekiti wa CHADEMA taifa (2025-2029).

Aliongeza kuwa kwenye nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Hemed alisema kwa kuangalia nani mwenye uzito wa kipekee wa taifa na anaweza kuendeleza harakati za mageuzi kwenye vyama vya siasa, wao wanatupa karata yao kwa John Heche.

Aidha, alisema kwamba wanawashauri wajumbe wa chama hicho kutoka mkoa wa Tanga, kuangalia uelekeo sahihi, kwa sababu yametokea mengi ya vurugu vurugu kwa mkoani humo katika miaka ya nyuma na uongozi wa mkoa kuvurugwa na kuvunjwa bila kufuata taratibu za kichama.

Alisema ni wasaa wa kipekee kutafakati aina gani ya timu au watu wa kuivusha CHADEMA kwenye hilo ombwe la kisiasa lililopo wana mambo mengi, ikiwamo watu wanatekwa lakini hawaoni kauli za viongozi kulikemea hilo.

"Wanaona viongozi wa vyama vyengine vya siasa wakitekwa na kuuawa, wakiumizwa hawaoni uzito wowote unaochukuliwa kwenye hilo. Kwa hiyo pia nawaasa viongozi wa vyama vya siasa, sio tu kupigania maslahi ya uongozi hata wananchi," alisisitiza.

Aidha, alisema kwa aina ya watu kama Lissu wanahitajika kwenye kipindi walichonacho kigumu cha mkwamo wa kiasiasa, kwa kuwa kwa namna fulani ukiangalia uchaguzi wa serikali za mitaa umefanyika ubabaishaji, hivyo kunahitajika damu mpya na nguvu kubwa katika mabadiliko.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokasia Makini, Assey Shewaly, alisema maoni yake ambapo alianza na Mwenyekiti wa sasa wa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ni muhimili wa chama hicho, ambaye ameijenga kwa muda mrefu na anapaswa kushukuriwa sana kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Alisema kwa upande wake, anatamani Tundu Lissu amrithi Mbowe, kwa sababu ana mchango mkubwa kwenye chama hicho na mvuto kwenye siasa za nchi na harakati zake ndani ya chama. Alisema kutokana na hilo watu wanadhani anaweza akawa hana jipya na wakamchoka japo wakawa na mambo mazuri na kutokujua mchango wake.


Shewally, alisema ndani ya chadema mchango wake maoni yake utafiti alioufanya na mazingira ya siasa za nchi kwa sasa na hapo waliofikia lakini kabla ya mwaka 1992 watu wakigombea kwa vyama vyangi kuna hatua ya demokrasi imefikia nchini.

Alisema ukiangalia katika uchaguzi, wamerudi nyuma kwa asilimia 95 kwa hiyo siasa zimebadilika, lakini kwa siasa za sasa, Lissu anafaa zaidi.

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Balisidya alipotaka kuipindua Dar Jazz

**Na Adam Fungamwango**




Bendi ya Afro 70.

KWENYE tasnia ya muziki wa dansi, hasa wa zamani kuna hadithi nyingi sana zinazozungumzwa, zilizozungumzwa, lakini pia kuna zile ambazo hazijazungumzwa pia.

Pamoja na mashabiki wa muziki wa dansi hasa ule wa miaka ya kuanzia 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 kusikiliza na kufurahia muziki huo, bado kuna mambo mengi ambayo yamepitika na bado watu hawakuyajua.

Kwa sasa angalau mashabiki wamekuwa wakisikia maelezo mengi, kama vile muziki fulani ulipigwa kwa madhumuni gani, lakini inavyoonekana muziki huo bado una hadithi nyingi ambazo zitaendelea kuibuka vizazi kwa vizazi.

Labda wakati huo watu walikuwa hawajui kwa sababu hakukuwa na vyombo vingi vya habari na mitandao ya kijamii.

Kukosekana kwa wachambuzi siku za nyuma ambayo wangekuwa na uwezo wa kudodosa hili na lile, nalo liliwanyima nafasi mashabiki kujua vitu vingi.

Kwa sasa kuna habari na hadithi nyingi zinajitokeza na kuzungumza hadi mtu unashangaa.

Mfano, bendi ya Bana Ngenge ambayo ilitisha sana miaka ya 1980 nchini Kenya, kumbe ilikuwa nchini Tanzania na kulazimika kukimbilia nchini humo kwa kuikimbia Orchestra Safari Sound chini ya mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita' ikiongozwa na King Kiki.

Mmoja wa wanamuziki wa (OSS) hivi karibuni alikaririwa kwenye vyombo vya habari kuwa awali Bana Ngenge ndiyo ilikuwa ikipiga Safari Resorts. Lakini walipokuja wao awali walidharaulika, lakini baadaye Bana Ngenge aliona moto ni mkali wakakimbia nchi.

Si wengi wanaojua kuwa kumbe Ndala Kasheba alikuwamo kwenye kikosi cha OSS Masantula Ngoma ya Mpwita ya Kiki kama mwanamuziki wa kawaida, akiwa na mkwe wakati huo, Bakambi Nkela ambaye naye alikuwa mwimbaji.

Wengi wanajua kuwa Kiki alipoondoka ndiyo akaja Kasheba. Ukweli ni kwamba awali Kasheba alikuwepo kwenye kikosi cha kwanza, lakini kabla ya kurekodi akaondoka yeye na mkewe kwenda nchini Burundi kimuziki.

Baada ya mkataba wa Kiki na OSS kumalizika, ndipo mmiliki wa bendi hiyo, Hugho Kisima alipomrudisha Kasheba ambaye aliasisi mtindo wa Dukuduku.

Nadhani si mashabiki wengi pia wanaofahamu kuwa mwimbaji Lovy Longomba aliyewika nchini Kenya na Super Mazembe akaja nchini kujiunga na bendi ya African Sound 'Afriso Ngoma', ameshawahi kuimbia Maquiz Original na Bicco Stars kwa vipindi vifupi.

Kabla ya kuingia Afriso alikuwa Maquiz, lakini alidakwa na mmiliki wa bendi hayati Juma Mwendapole na kumpeleka kwenye bendi yake.

Kabla ya kuunda bendi yake ya Super Lovy alipotoka Afriso, mwanamuziki huyo mwenye sauti nyororo alijiunga Bicco Stars alifuata rafiki yake Ramadhani kinguti kwenye sauti nzito na alikuwa naye Afriso. Wengi hawajui habari hizo kwa sababu huko alikopitia hakurekodi.

Hata mpiga solo marehemu Mosesengo Fanfan ambaye wengi nchini wanajua alizipigia bendi ya Super Matimila na Orchestra Makassy, aliwahi kujiunga na Maquiz Original, lakini aliondoka kabla ya kurekodi, ndiyo maana wengi hawajui.

Leo nawapa hadithi ya bendi kongwe ya Dar Jazz ilivyotaka kupinduliwa na bendi yake ya kikosi cha pili.

Zamani bendi nyingi zilikuwa na vikosi vya pili kama timu za mpira wa miguu. Kikosi cha pili cha Dar Jazz kilipata mwanamuziki Patrick Balisidya. Hakuweza kuwemo kwenye kikosi cha kwanza kwa sababu kulikuwa na mkongwe King Michael Enock ambaye alikuwa akipiga solo.

Balisidya alipiga solo na kuimba. Ilikuwa mwishoni mwa miaka ya 1960, Dar Jazz ilikuwa ikifanya onyesho kwenye kumbi moja Dar es Salaam. Cha ajabu watu walikuwa ni wachache na si kawaida.

Muda mfupi baadaye ikaja taarifa kuwa mashabiki wengi wa Dar Jazz wamefurika kwenye onyesho la Dar Jazz B. Hiyo ilimshtua King na mmiliki wa kundi hilo.

Kumbe Balisidya alipopelekwa kwenye kikosi cha pili, alitumia kipaji chake cha kupiga solo na kuimbaji kukibadilisha kikosi hicho na kuwa tishio si kwa Dar Jazz pekee, bali hata baadhi ya bendi zingine.

King akamwambia mmiliki kuwa bila kuua bendi hiyo, Dar Jazz kubwa itapata shida sana kwa sababu mashabiki wameshatokea kuikubali na kupenda muziki wake.

Ni kwa sababu bendi hiyo ilipiga miziki yenye staili zote za kisasa na kizamani. Ilipiga miziki ya kizungu kama ile ya kina James Brown, Kikongomani, mtindo kama ya Dar Jazz yenyewe kubwa, halafu wakatunga na kuimba nyimbo zao kisasa zaidi, hivyo kufanya mashabiki kuanza kuikacha bendi kubwa.


Mmiliki akavunja kikosi cha pili cha Dar Jazz. Wale wanamuziki walioonekana wakali, kama Balisidya na wengine wachache wakapandishwa kwenye kikosi cha kwanza.

Hii ilimuuma sana Balisidya kwani alishaanza kutengeneza kama utawala wake hivi na umaarufu.

Kwa jinsi alivyoteka mashabiki, aliona ilikuwa ndiyo njia yake ya kutengeneza jina.

Hata hivyo ilimfunza kitu. Alijiona kumbe anaweza, hivyo lake lilikuwa rohoni.

Aliendelea kupiga Dar Jazz, lakini akiwa na sononeko moyoni hadi aliposaidia na baba yake mzazi kununua vyombo na kuunda bendi ya Afro Band, ambayo ilijulikana kama Afro 70 kutokana na kuundwa miaka hiyo na kujipatia umaarufu mkubwa.



Patrick Balisidya

HABARI KIMATAIFA

# Trump ajiandaa kukutana na Putin

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS mteule wa Marekani Donald Trump, amesema maandalizi yanaendelea kwa ajili ya mkutano wake na Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Uingereza, REUTERS, mkutano huo bado haujafahamika wapi na lini utafanyika.

"Yuko tayari kukutana, na tunafanya maandalizi," Trump aliwaambia waandishi wa habari kabla ya kukutana na magavana wa chama cha Republican katika makazi yake ya Mar-a-Lago katika jiji la Florida.

"Rais Putin yuko tayari kukutana. Amesema hayo hadharani, ni lazima tukomeshe vita hivi," alisema Trump.

Akizungumzia vita vya Ukraine, aliahidi kuvimaliza lakini hajaweka bayana ni njia gani hasa amepanga kuzitumia.

Ikulu ya Russia Kremlin bado haijazungumza kuhusua kauli ya Trump, lakini siku moja kabla, msemaji wa rais wa Russia, Dmitry Peskov aliwaambia waandishi wa habari, ikiwa Trump ataendelea na nia yake ya kutaka kuzungumza na rais wa Vladmir Putin baada ya kuapishwa, Mrussia inakaribisha hilo.

Peskov alisema kuwa hadi sasa hakuna maombi ya mkutano kama huo kutoka upande wa Marekani.

Hata hivyo, Putin mwenyewe alisema mwezi Desemba kwamba yuko tayari kukutana na Trump.

**BBC**



Vikosi vya kuzima moto vya angani na ardhini vikipambana na moto unaendelea kuteketeza eneo kubwa la Los Angeles katika jimbo la California na kusababisha vifo vya watu 10. **PICHA: AFP**

# Kagame asisitiza hahusiki na mgogoro nchini DRC

**RWANDA**

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, amesisitiza kwamba wapiganaji wa Kundi la M23 wanaopigana ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hawafadhiliwi na serikali yake kama inavyodaiwa.

Kiongozi huyo alieleza kuwa vita vinavyoendelea katika eneo hilo la mashariki mwa DRC ni matokeo ya nchi zilizotawala eneo hilo.

"Vita vimeendelea kwa miaka mingi. Je, watu hapa hawajui jinsi vita hivi vilivyoanza? Vita hivi vilianza miaka mingi iliyopita na haikutokana na Rwanda." Alisema Rais Kagame.

Aliongeza kuwa vita hivyo vilianzishwa na makundi yalikuwapo DRC na huenda baadhi yao wana asili ya Rwanda lakini walikuwa wamehamia nchini humo tangu enzi za ukoloni.

Rais Kagame alisema kuwa ingawa viongozi wa DRC wameonekana kukiri kuwa waasi hao ni Wakongo lakini cha kushangaza wanadai kuwa vita hivi vinaungwa mkono na Rwanda.

Kauli ya Rais Kagame inajiri baada ya waasi wa M23 kuchukua udhibiti wa mji wa Masisi siku tatu zilizopita.

Rwanda inadaiwa kutumia kundi la M23 kupora madini kutoka mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kama vile dhahabu, cobalt na tantalum, ambayo hutumiwa kutengeneza simu za mkononi na betri za magari yanayotumia umeme.

Mwezi uliopita, DRC ilisema inaishtaki kampuni ya kununua madini yanayopatikana kwa njia haramu na kuifanya kampuni hiyo kubwa ya teknolojia kusema kuwa imeacha kutumia madini kutoka katika nchi hizo mbili.

Rwanda imekanusha kuwa mshirika wa usafirishaji wa madini haramu kutoka DRC.

# Uturuki yakana kuchukua eneo Syria

**ANKARA,** UTURUKI

UTURUKI imesema haina nia ya kulichukua eneo lolote la Syria kufuatia kuondolewa madarakani Bashar al-Assad.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Hakan Fidan, wakati akizungumza na waandishi habari mjini Istanbul.

Wasiwasi umekuwa ukiongezeka kuhusu kitisho cha Uturuki dhidi ya vikosi vya Kikurdi vilivyopo katika nchi hiyo iliyoharibiwa kwa vita.

Wakati huo huo, mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Kaja Kallas, alisema umoja huo unaweza kupunguza hatua kwa hatua vikwazo vya Syria ikiwa maendeleo yataonekana.

Kallas alisema vikwazo hivyo vinaweza kuondolewa iwapo viongozi wapya watachukua hatua za kuunda serikali yenye kuyashirikisha makundi yote na inayowalinda watu wachache.

# DRC yafunga kituo cha Al Jazeera

**KINSHASA,** DRC

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imekipiga marufuku kituo cha televisheni cha Al Jazeera kuendesha shughuli zake nchini humo baada ya kufanya mahojiano na kiongozi wa kundi la waasi la M23.

Kwa mujibu wa msemaji wa serikali ya DRC, Patrick Muyaya, mamlaka ya nchi hiyo ilibatilisha kibali cha waandishi wa shirika hilo kuwapo nchini humo.

Jumatano ya wiki hii kituo cha televisheni cha Al Jazeera, kilimuhoji Bertrand Bisimwa, Mkuu wa kundi la waasi la M23 linalopambana na jeshi mashariki mwa nchi hiyo.

Katika mahojiano hayo Bisimwa, aliishutumu serikali ya DRC kwa kukiuka makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyofanyika mwezi Agosti na kudai kwamba kundi la M23 linaendesha vita kamili.

Muyaya aliyafananisha mahojiano hayo kuwa sawa na kuukumbatia ugaidi na kwamba hilo halikubaliki na kuwataka wanahabari kutotoa fursa kwa magaidi.

"Niliamua, baada ya tathmini na mashauriano na timu yangu, kuondoa vibali vilivyotolewa kwa waandishi wa habari wa Al-Jazeera," alisema Muyaya mbele ya waandishi wa habari.

Aliongeza kwamba mara zote waandishi wa habari wameidhinishwa kufanya shughuli zao nchini humo, lakini kwa awamu hii kituo hicho kimekiuka kwa kuongea na mtu anayeiunga mkono Rwanda.

"Wanawezaje kutumia mtafiti, ambaye ni mwanaharakati anayejulikana anayeunga mkono Rwanda ambaye hayumo kwenye orodha ya waandishi wa habari walioidhinishwa ambao wanamhoji kiongozi wa vuguvugu la kigaidi bila ya kuwa na kibali au viza. Je, hiyo si dharau? " alihoji.

Saa chache kabla ya kauli ya msemaji huyo wa serikali, Waziri wa Sheria Constant Mutamba, kupitia mtandao wa X aliandika kwamba mtu yeyote anayeripoti kuhusu shughuli za jeshi la Rwanda na wasaidizi wake M23 watakabiliwa na mkono wa sheria akimaanisha adhabu ya kifo.

Hata hivyo andiko hilo halikupewa msisitizo na msemaji wa serikali na badala yake alisema kauli ya waziri ililenga mtu anayeweza kumtumikia adui.

Hata hivyo, upinzani nchini humo umekosoa serikali ya DRC kukifungia kituo hicho na matamshi ya kutishia wanahabari.

Kupitia mtandao wa X msemaji wa upinzani, Hervé Diakiese, alisema uhuru wa kujieleza unamaanisha uwezo sio tu wa kueneza propaganda za serikali bali pia mambo yanayoweza kuchukiza na kusababisha madhara.

**DW**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Waziri wa Nchi anayeshughulikia Kilimo, Mifugo na Uvuvi Uganda, Fredrick Bwino Kyakulaga, alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebbe nchini humo jana, ambako atamwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano kuhusu Mpango wa Kilimo Afrika utakaofanyika leo. Kushoto ni Balozi wa Tanzania Uganda, Meja Jenerali Paul Kisesa na (kulia) ni Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Kanali Mstaafu Fredy Mwesigye. **PICHA: OWM**



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia) pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (kushoto), wakiingia katika Studio za TBC 1 kufanya mahojiano kuhusu Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika. **PICHA: ONWM**



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akiagana na Balozi wa Marekani nchini aliyemaliza muda wake, Michael Battle, baada ya kikao chao, jijini Dodoma jana. **PICHA: WF**



Aliyekuwa Balozi, Dk. Wilbroad Slaa, akiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka ya kusambaza taarifa za uongo kwenye mtandao wa X. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# HADITHI

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumwona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumwangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo hukupata kudhani.
Unaweza kukutana na mtu ambaye kwa mwonekano na jinsi anavyokutendea ukamwona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana.
Kwenye kijiji kimoja kilichoko Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini.
Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa.
Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je, muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

# Malaika shetani-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




"Sababu hasa ya kumuua huyo binti ni nini?" Mmoja akauliza. Yule aliyeonekana ndiyo anawatuma akamtazama kwa macho makali.

"Wewe siyo mtaalamu wa mambo haya eee. Umeanza lini hii kazi? Halo! Akawageukia wenzake wawili, huyu ameanza lini hii kazi? Huwa hatuulizi kwa nini. Umepewa tenda ya kuua mtu au kumdhuru, unachotakiwa kufanya wewe ni kuhakikisha malipo yako yanakamilika kwa jinsi mlivyoahidiana, siyo kuuliza sababu. Haya kama ukiambiwa sababu ndiyo unakwenda kumponya, au kumuua mara mbili?" Hakuna aliyejibu. Walibaki wamtazama.

"Ni hivi, kila mmoja amepata chake. Kila mmoja amepata nusu ya malipo. Kila mmoja ana shilingi laki tatu hapo nimeshawapa, na kazi ikimalizika mnamaliziwa laki mbili kila mmoja. Hilo ndilo la muhimu. Sababu huwezi kuijua. Mimi mwenyewe hapa siijui sababu ya kuuawa huyu denti Naima. Kuna bosi amenipa hii tenda na wala sijamuuliza kwa nini. Ameniambia nitafute vijana wa kazi, nimewapata nyinyi, najua mtaifanya. Kisa nini? Atajua mwenyewe, hapa kila mmoja amepata chake, maisha yanaendelea. Kama siku nyingine atakuwa na mtu mwingine anataka kumfuta kwenye uso wa dunia, ataniita na mimi nitawafuata," alisema na kueleweka.

Kikubwa hapo ni kwamba hata aliyewatuma vijana wataokwenda kutekeleza mauaji ya Naima naye hajui kisa chochote. Amebebwa na tamaa ya pesa tu.

Walikutana chini ya mti mmoja mkubwa, maeneo ya kando ya kijiji cha Mikwambe na Matuo. Walikana hapo ili mipango yao isivuje na kujulikana. Na wakaahidiana baada ya tukio watakutana tena hapo kwa ajili ya kumaliziana malipo yaliyobaki.

Wauaji hao wote walikuwa wametoka kwenye vijiji tofauti vya mbali. Baada ya kupatikana mmoja, alianza kuwakusanya wenzake anaowafahamu, ambao huwa wanatumiwa na watu mbalimbali wabaya kuwadhuru, kuwaumiza au kuua watu kwenye vijiji mbalimbali huko Bungu.

Kama walivyopanga. Walifika maeneo hayo saa 11:00 jioni na kujitomeka kwenye vichaka vya pori hilo kwa nina ya kumsubiri Naima. Ilitimia saa 12:00 hivi na dakika zake, Naima alikuwa anatoka zake Matuo alikuwa tayari ameshaingia kijijini kwao Bungu. Ni vijiji ambavyo vilikuwa salama na amani. Hakuna matuko yoyote mabaya ambayo yanatokea kwenye kijiji hicho. Pamoja na kwamba kina wanyama, lakini hakina wanyama wa hatari ambao wanashambulia watu.

**Mwili wake umekutwa kwenye pori la kijiji hicho, ukiwa umepigwa vibaya na umezikwa nusu. Yaani kuna upande ulikuwa umefukiwa na upande mwingine haukufukiwa.**

Ndiyo maana wanavijiji wa jirani wamekuwa wana wasiwasi na kutembeleana, hata wanawake hawaogopi kutembea peke yao kutoka kijiji kimoja kwenda kingine.

Ghafla vijana watatu wakajitokeza. Walikuwa wameshika silaha za jadi. Hakuonekana kuwa na mzungumzo mengi au kuuliza maswali. Kazi waliyotumwa ni moja tu. Kuhakikisha wanatoa uhai wa Naima. Wanaume katili watatu hawakuchukua hata dakika mbili kuhakikisha wamemmaliza binti hiyo.

Kuna maswali ambayo watu walikuwa wanajiuliza kijijini baada ya kupatikana kwa mwili wa Naima.

Mwili wake umekutwa kwenye pori la kijiji hicho, ukiwa umepigwa vibaya na umezikwa nusu. Yaani kuna upande ulikuwa umefukiwa na upande mwingine haukufukiwa.

Wauaji walifanikiwa kumuua, lakini hawakufanikiwa kumfukia. Lengo inaonekana ni kumuua na kumfukia. Kumfukia kwao ilikuwa ni kuua ushahidi. Wangefanikiwa ina maana Naima ingesemekana amepotea. Ametoweka, hivyo ingewapa kazi wanakijiji kumsaka huku na huko bila mafanikio. Hawakufanya hivyo. Inaonekana si kwa bahati mbaya. Kuna kitu ambacho kimesababisha kutimiza lengo lao muhimu kabisa la kupoteza ushahidi. Kwa wauaji, kutoa roho ya mtu ni jambo dogo sana. Kazi kubwa inabaki kupoteza ushahidi ili waofuatilia, iwe wananchi, raia au askari polisi walianza upelelezi wao washindwe kupata chochote kitakachowapeleka mbele ya mauaji. Inaonekana ni kama walikimbia. Inawezekana kulikuwa na mtu anapita eneo la tukio muda ambao wanaanza kumfukia, ndipo waliamua kukimbia. Hata hivyo wapo wanaojiuliza, ni kwa nini alipopita hawakurudi kuendelea na kazi yao? Wengine wanajiuliza wauaji waliokuwa na roho ya kikatili kumuua Naima kwa nini wakawa na roho nzuri kutomuua yule ambaye aliwakuta wanamfukia?

Ni kweli kabisa. Wakati wanachimba shimo ili kufukia maiti, kuna mtu alipita maeneo yale. Ilionekana kabisa kuwa alikuwa ameshaona kitu ambacho si cha kawaida, hivyo alipita kwa kunyata. Hata hivyo aligusa kijiwe ambacho kiporomoka kutoka juu na kusababisha sauti ya majani ambayo iliwaashiria kuwa kulikuwa na mtu karibu yao. Mtu yule alikuwa anapita au ananyaka kuangalia nini wanakifanya.

Walichofanya walikurupuka na kuanza kumkimbiza. Alionekana kuwa na mbio kuliko wao.

Kitu pekee walichofanikiwa kufahamu kutoka kwake, ni kwamba alikuwa kijana mwenye umri wa miaka 23 mpaka 25 hivi. Alivaa fulana nyeusi na jinsi lililochakaa la bluu. Aliwachezesha mdundiko kwenye pori na hatimaye hawakumuona tena. Iliwachukua kama nusu saa kumsaka. Walipochoka kufanya kazi hiyo, walikutana na kuamua kutorejea tena eneo walilofanya mauaji kwa kuhofia kukamatwa. Huwezi kujua aliyewaona anaweza kwenda kuwaambia watu kwenye vijiji wakaja na kuwakuta wanafanya kazi ya kufukia maiti. Huwezi kujua labda wakati wanamfukuza kuna mtu mwingine alipita na kuona maiti na kwenda kuita watu. Ilikuwa ni hatari kuendelea kuifukia. Walichofanya wakatimka kila mmoja. Kazi ya kuua wameshaifanya. Ambacho hakikufanyika ni kuondoa ushahidi. Kuufukia mwili wake. Ungefukiwa haya yote yasingetokea. Kijiji kingekuwa na kazi moja tu ya kumtafuta. Wanakijiji wangeweza hata kutumia mwezi mzima kufanya kazi hiyo asijulikane ameenda wapi. Inawezekana kungeazishwa hata propaganda kuwa ametoroshwa na mwanaume. Mwanzoni wangeweza kukataa kwa sababu ya tabia yake njema, lakini baadaye kuna watu wangeanza kuunga mkono. Walifanya tukio hilo wangeweza hata kutembeza pesa ili propaganda hiyo ienee na kusadikiwa. Baadaye wazazi wake wangeendelea kumsubiri mtoto wao bila mafanikio. Hiyo ingekuwa salama na wauaji na mtu aliye nyuma ya pazia.

Badala yake wanakijiji wamekuja juu, wanataka kazi ya kusaka wauaji ianze mara moja.

*Itaendelea Jumamosi*

# MBEYA CITY YAZIDI KUSHUSHA 'MAJEMBE' CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City, imeendelea kufanya usajili wa kuboresha kikosi chake katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili na kuzitisha timu za Ligi ya Championship.

Klabu hiyo inayohangaika kurejea Ligi Kuu baada ya kuteremka msimu wa 2022/23, jana imetangaza kusajili wachezaji wanne ambapo imesema itakifanya kikosi kuwa bora zaidi na kuweza kukirudisha Ligi Kuu msimu ujao.

Mbeya City ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi ya Championship, ikiwa na pointi 31, nyuma ya Mtibwa Sugar inayoongoza ikiwa na pointi 35, timu zote zikiwa zimecheza michezo 14.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo inasema kuwa wachezaji waliosajiliwa ni kiungo mkabaji, Stewart Sweetbeth na Beki Said Mashoto wote kutoka Biashara United, kiungo mshambuliaji, Daniel Lukandamila kutoka Tabora United na Bruno Shayo ambaye ni kiungo mshambuliaji kutoka Stand United.

Siku chache zilizopita klabu hiyo ilitangaza kuwasajili kipa wa Biashara United, Diey Makonga na straika, Kelvin George, Mtanzania aliyekuwa anacheza soka la kulipwa katika klabu ya AS Port ya Djibouti.

Klabu hiyo imesema bado inaendelea kuangalia ni sehemu gani zenye mapungufu ili kuleta maingizo mapya ambapo imedhamiria kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

Timu hiyo ilishuka daraja msimu wa 2022/23, baada ya kufanikiwa kupanda na kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu wa 2013/14 na kuwa moja kati ya timu tishio kwenye Ligi wakati huo.




Msemaji wa zamani wa klabu ya Yanga ambaye kwa sasa ni balozi wa Yas, Haji Manara (katikati), akiwa pamoja jana na washindi wa shindano la magifti, kulia ni Meneja wa Wateja Maalum wa kampuni hiyo, Mary Rutta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watatu waanza mwaka kwa ushindi

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wa tatu wajanja wametangazwa washindi katika shindano la magifti linaloendeshwa na kampuni ya Yas.

Wajasiriamali hao kila mmoja amejishindia fedha shilingi milioni moja ambazo wamesema watazitumia kukuza biashara zao.

Mmoja wa washindi hao, Halina Saidi ambaye ni mfanyabiashara wa nguo za mitumba, alisema fedha alizozipata atazitumia kuongeza mtaji kwenye biashara yake hiyo.

"Kwa kweli nawashukuru sana Yas, fedha hizi zimekuja wakati muafaka nikiwa napambana na biashara yangu, zitaenda kunisaidia kuongeza mtaji," alisema.

Aidha, mshindi mwingine, Rehema Salum ambaye ni mfanyabiashara wa samaki Chamazi jijini Dar es Salaam, alisema awali hakuamini alipopewa taarifa za kushinda fedha hizo.

"Nilikuja kuamini nilipoambiwa nije kwenye ofisi za Yas, nashukuru sana na kwa kweli, nimeuanza mwaka vizuri," alisema Rehema.

Aidha, balozi wa kampeni hiyo ya magifti, Haji Manara, aliwataka wananchi kushiriki kampeni hiyo kuweza kushinda zawadi mbalimbali.

"Hizi zawadi zinatolewa kweli, watanzania wenzangu washiriki kwenye kampeni hii kuweza kushinda kama hawa walioshinda leo," alisema Manara.

Kwa upande wake, Meneja wa Wateja maalum wa kampuni hiyo, Mary Rutta aliwapongeza washindi hao wa wiki ya sita ya kampeni hiyo.

# Beki wa Yanga atua Tabora United

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa kushoto wa klabu ya Yanga, Yassin Mustafa, yuko katika hatua za mwisho kukamilisha usajili wa kujiunga na Tabora United.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mazungumzo baina pande mbili yamefikia pazuri na mchezaji huyo anatarajiwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kuongezwa kipindi cha dirisha dogo la usajili kinachotarajiwa kufungwa Jumatano ijayo.

"Hatua hii ya kumsainisha beki huyu inatarajiwa kuimarisha safu yetu ya ulinzi ya Tabora United katika mashindano mbalimbali. Yasini anajulikana kwa uwezo wake wa kudhibiti mashambulizi ya wapinzani na kuchangia kwa kasi katika mashambulizi ya pembeni, tunatarajia atakuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi chetu," alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo ambaye hakutaka jina lake ltajwe.

Tabora inamsajili mchezaji huyo akitokea Mtibwa Sugar ambayo kwa sasa inashiriki Ligi ya Championship.

Beki huyo alitamba akiwa na Yanga alipojiunga mwaka 2022, kabla ya kutimkia Singida Big Stars, ambayo baadaye ilibadilishwa jina na kuitwa Fountain Gate.

Mbali na beki huyo wa kushoto, taarifa zinasema klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kipa raia wa Gabon, Jean Noel Amonone aliyewahi kuzichezea klabu ya Amazulu ya Afrika Kusini na AS Arta Solar ya Djibouti ili kuchukua nafasi ya Hussein Masalanga anayejiandaa kurejea kwenye klabu yake ya Singida Black Stars.

Masalanga yupo Tabora United kwa mkopo akitokea Singida Black Stars ambayo imeanza kurejesha wachezaji wake kipindi hiki cha dirisha dogo kama Marouf Tchakei, ambaye awali naye alikuwa Tabora United.

Tabora United imefanya vizuri kwenye mzunguko wa kwanza ikiwa inashika nafasi ya tano baada ya kukusanya pointi 25.

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### RASHFORD ATAKIWA WEST HAM
WEST Ham inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa England, Marcus Rashford na wanataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa mkopo kutoka Manchester United. ***(Talksport)***

### MAN YAMTAKA KVARATSKHELIA
KLABU ya Manchester United iko tayari kuchuana na Paris St-Germain kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Georgia, Khvitcha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23. ***(L'Equipe)***

### RASHFORD AWA LULU SERIE A
KLABU za Serie A, AC Milan na Como zina nia ya kumsajili Marcus Rashford kwa kipindi kilichosalia cha msimu huu. ***(Gianluca Di Marzio)***

### WANNE WAVUTIA EPL
NYOTA wanne wa Bournemouth wanavutia klabu za Ligi Kuu England, huku Illia Zabarnyi, Milos Kerkez, Antoine Semenyo na Dean Huijsen wakifuatiliwa na Chelsea, Newcastle United na Liverpool. ***(I)***

### UNITED YAMWINDA MBEUMO
KLABU ya Manchester United imeungana na Arsenal katika mbio za kumnunua mshambuliaji wa Cameroon, Bryan Mbeumo mwenye umri wa miaka 25 kutoka Brentford. ***(Mirror)***

### MAN CITY KUMSAJILI REIS
MANCHESTER City inafanyia kazi mpango wa kumsajili beki wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, Vitor Reis kutoka Palmeiras. ***(Athletic)***

### DOUGLAS LUIZ KUTUA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imemuulizia mchezaji wa Juventus, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 26, lakini kiungo huyo wa kati wa Brazil anawaniwa na Manchester United, Manchester City na Fulham. ***(Mail)***

### NEWCASTLE YAMTAKA RAMSDALE
GOLIKIPA wa Southampton na England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 26, anafuatiliwa na Newcastle United. ***(Sun)***

### ALLEYNE AWANIWA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inamtafuta mlinzi wa Manchester City mwenye umri wa miaka 19, Max Alleyne. ***(Fabrizio Romano)***

### KLABU MBILI ZAMTAKA ELLIOTT
KIUNGO wa kati wa Liverpool na England, Harvey Elliott mwenye umri wa miaka 21, ananyatiwa na klabu za Brighton na Borussia Dortmund. ***(Lyall Thomas)***

### MITCHELL AWINDWA ENGLAND
TYRICK Mitchell wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 25, anasakwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England na beki huyo pia amekuwa akiwindwa na Atletico Madrid. ***(Mirror)***

### GOMIS AWANIWA VILLA
KLABU ya Aston Villa inajadiliana na klabu ya Ligue 2 ya Caen kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Tidiam Gomis mwenye umri wa miaka 18. ***(L'Equipe)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RASHFORD KUBADILISHANA NA KVARATSKHELIA WA NAPOLI

Nyota huyo Mwingereza amepoteza namba kwenye kikosi cha kwanza chini ya kocha Amorim na wanataka ku...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imefanya mawasiliano na Napoli kuhusu mpango wa kubadilishana Marcus Rashford na Khvicha Kvaratskhelia, kwa mujibu wa ripoti.

Akiwa amepoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza chini ya kocha mkuu, Ruben Amorim, Rashford anapatikana kwa uhamisho mwezi huu, lakini United bado haijapokea ofa yoyote isipokuwa nia ya mkopo kutoka kwa pande ambazo haziwezi kukidhi mahitaji yao ya kifedha.

AC Milan wametawala vichwa vya habari, lakini Rashford anaweza kujikuta akielekea sehemu nyingine ya Italia huku mazungumzo yakiendelea na Napoli kuhusu mpango wa kubadilishana wachezaji.

Napoli wameripotiwa kuwa tayari kumuachia Kvaratskhelia na wanasemekana anafanya mazungumzo na United kuhusu uwezekano wa kubadilishana na Rashford, ambaye ni mmoja wa walengwa wa kocha Antonio Conte ili kuimarisha safu yake ya mashambulizi.

Jambo linalotia ugumu zaidi kwa United ni kwamba PSG wanataka kumnunua Kvaratskhelia ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Georgia katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Fabrizio Romano amebainisha kuwa Napoli pia wanawasiliana moja kwa moja na PSG ambao wanapendekeza mpango wao wa kumbadilisha na beki wa kati, Milan Skriniar.

Napoli wamempa Kvaratskhelia mkataba mpya, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika 2027, bado hajatoa jibu kwani anapima chaguzi zote zinazowezekana kwake.



# Ancelotti: Ugomvi wa wachezaji haukuwa wa lazima

**JEDDAH, Saudi Arabia**

CARLO Ancelotti aliutaja ugomvi wa uwanjani kati ya wachezaji wa Real Madrid na Mallorca kuwa "usio wa lazima" baada ya ushindi wa 3-0 wa Madrid katika nusu fainali ya Supercopa ya Hispania huko Saudi Arabia, Alhamisi.

Jude Bellingham aliiweka Madrid mbele dakika ya 63 mjini Jeddah kabla ya bao la kujifunga la beki wa Mallorca, Martin Valjent na mkwaju wa dakika za mwisho kutoka kwa Rodrygo Goes ulihakikisha timu hiyo kufuzu fainali.

Wachezaji wote walivutana mashati uwanjani baada ya bao la Rodrygo, huku beki wa Mallorca, Pablo Maffeo ambaye mara kwa mara alikwaruzana na Vinícius Júnior wakati wa mechi alikwidana na Bellingham na kisha Raúl Asencio aliyetokea benchi kabla ya Ancelotti kuingia uwanjani kutuliza vurugu.

"Nilijaribu kutuliza mambo kidogo na Maffeo," alisema Ancelotti akiiambia Movistar.

"Niliingia uwanjani kusaidia kumaliza pambano hilo. Wachezaji walikasirika, lakini mwishowe hakuna kilichotokea."

"Vuruguzu zile hazikuwa za lazima," alisema Ancelotti baadaye katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Mchezo ulikuwa umekwisha. Siwalaumu wachezaji wangu au wachezaji wa Mallorca, haikuwa lazima kwa timu zote mbili."

"Kuna mchezaji wa Mallorca (Maffeo) ambaye tuna matatizo naye katika kila mchezo."

Kiungo wa kati Aurélien Tchouaméni, ambaye aliondolewa kama tahadhari baada ya mgongano wa vichwa, aliiambia Movistar baada ya mchezo.

"Watu walikasirika lakini jambo muhimu zaidi ni kushinda. Hatutaki kuzungumza juu ya mtu huyu kwa sababu ndicho anachotaka."

"Sijui, nilikuwa nalenga mwisho wa mechi," kocha wa Mallorca, Jagoba Arrasate alisema.

"Sijui nini kilitokea, wachezaji wetu walikuwa na hasira kuhusu mabao hayo mawili, nadhani. Nilikuwa mbali sana."

Madrid itacheza na Barcelona kwenye fainali ya michuano hiyo Jumapili ijayo baada ya Barca kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Athletic Club katika nusu fainali ya kwanza Jumatano.

# Ronaldo afunga bao mwaka wa 24 mfululizo

**RIYADH, Saudi Arabia**

CRISTIANO Ronaldo alifungua akaunti yake ya mabao kwa mwaka 2025 Alhamisi, ikiwa ni mwaka wa 24 mfululizo kufunga katika soka la kulipwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 alifunga kwa mkwaju wa penalti kwa bao la pili la Al Nassr katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Al Okhdood kwenye Ligi ya Saudia (SPL), huku mabao mengine mawili yakifungwa na fowadi wa zamani wa Liverpool, Sadio Mané.

Ronaldo aliandika kwenye ukurusa wake wa X kusherehekea ushindi huo, akiandika: "Njia bora ya kuanza mwaka."

Mabao yake ya kwanza alifunga Oktoba 2002 akiwa na Sporting CP, akifunga mara mbili wakati timu yake ilipoishinda Moreirense kwenye Ligi Kuu ya Ureno.

Tangu wakati huo, amefunga zaidi ya mabao 900 katika maisha yake ya soka akiwa na Sporting, Manchester United, Real Madrid, Juventus, Al Nassr na timu ya taifa ya Ureno.

Ushindi wa Al Nassr uliwarudisha hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa SPL na wana pointi sawa na Al Qadsiah ambao wana mchezo mmoja mkononi.

Kikosi hicho cha kocha, Stefano Pioli kipo pointi nane nyuma ya viongozi Al Ittihad, ambao pia wana mchezo mkononi.

# MAN CITY YASAKA WALINZI WA KATI

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imepiga hatua za haraka katika kumsaka beki wa kati wa Palmeiras, Vitor Reis, huku kukiwa na ripoti kwamba wameshakubaliana kuhusu maslahi binafsi na Mbrazil huyo.

Beki wa Lens, Abdukodir Khusanov pia amebakia kwenye orodha ya matamanio ya klabu hiyo katika dirisha la usajili la Januari hii.

Ripoti nyingi, zikiwamo za BBC Sport, zimewataja Reis na Khusanov kama walengwa wa Januari hii na wote ni mabeki wa kati na wapo mwanzoni mwa safari zao za soka.

Kwa mujibu wa ripoti ya mazungumzo na Palmeiras yanaendelea na Reis anaweza kupatikana kwa euro milioni 40.

Reis atafikisha umri wa miaka 19 mwishoni mwa mwezi huu na bado yuko nje ya safu ya Palmeiras ambayo hivi majuzi imewaondoa Endrick na Estevao Willian aliyejiunga na Chelsea.

Man City hapo awali ilifanya biashara na klabu hiyo ya Brazil ili kumpata kinda Gabriel Jesus Januari 2017.

Katika umri wa miaka 20, Khusanov amekuwa nchini Ufaransa tangu 2023, akijiunga na RC Lens kutoka Energetik-BGU ya Belarusi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uzbekistan, ambaye angekuwa wa kwanza kutoka nchi hiyo ya Asia ya kati kucheza Ligi Kuu ya England pia ana thamani ya euro milioni 40.

City pia wanahusishwa na mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt mwenye thamani ya pauni milioni 50, Omar Marmoush na nyota wa Bayern Munich, Jamal Musiala.

Majira ya baridi haya yatakuwa ya mwisho ambayo Mkurugenzi wa muda mrefu wa soka, Txiki Begiristain atasimamia kabla ya kuondoka na kukabidhi mikoba kwa Hugo Viana.

# AHOUA HATARI MABAO MGUU WA KULIA LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, anaongoza kwa kupachika mabao kutumia mguu wa kulia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa iko mapumzikoni hadi Machi mwaka huu.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu za michezo, Ahoua, amepachika mabao saba kwenye Ligi Kuu mpaka sasa kwa kutumia mguu wa kulia.

Hiyo ina maana mabao yote saba ambayo ameyafunga mpaka sasa kwenye ligi, ameyapachika kwa kutumia mguu huo.

Mchezaji huyo raia wa Ivory Coast aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu kutoka klabu ya Stella d'Adjame, amepachika mabao saba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa nyuma ya kinara wa mabao, Elvis Rupia, raia wa Kenya anayeichezea, Singida Black Stars ambaye amefunga mabao manane.

Mastraika wawili, Clement Mzize wa Yanga na Selemani Mwalimu wa Fountain Gate, wamefunga mabao matano kila mmoja kwa kutumia mguu huo.

Hata hivyo, wachezaji wote hao wamepachika mabao sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Jumla ya wachezaji sita wanakamata nafasi ya tatu kwa kufunga mabao kwa mguu wa kulia.

Wachezaji hao ni Edger William wa Fountain Gate, Elvis Rupia wa Singida Black Stars, Paul Peter wa Dodoma Jiji, Idd Selemani ‚Nado' na Feisal Salum, wote wa Azam FC, na Marouf Tchakei ambaye mzunguko wa kwanza aliichezea Tabora United kwa mkopo na sasa amerejea kwenye klabu yake ya awali ya Singida Black Stars.

Hadi kumalizika kwa mzunguko kwanza, jumla ya mabao 264 yamefungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza huku baadhi ya timu zikiwa zimeshacheza mechi za kwanza za mzunguko wa pili.

Takwimu zinaonyesha kuwa mabao hayo yamefungwa kwenye michezo 127 iliyochezwa mpaka sasa.

Katika michezo hiyo, mechi 94 zimetoa washindi na 33 zimeishia kwa sare.

Katika michezo 94 ambayo timu zimeshinda, mechi 58 timu zimepatia ushindi zikicheza nyumbani na mechi 36 zimetoa washindi wakicheza ugenini.



Baadhi ya wachezaji wa Simba, Leonel Ateba, Yusuph Kagoma na Muzamir Yassin wakitoka kwenye uwanja wa ndege jijini Luanda, Angola, Simba kesho watacheza mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquiz ya nchini humo. **PICHA: SIMBA**

# Azam: Bado hatujamaliza usajili

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutangaza kumsajili beki wa kati raia wa Ivory Coast, Zouzou Landry, klabu ya Azam FC imesema haijamaliza kufanya usajili na wanajiandaa kushusha tena nyota wengine ambao wanahitajika na Kocha Mkuu, Rachid Taoussi.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema uliofanyika ni usajili wa mwanzo tu kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo na watafanya usajili mwingine ili kuendelea kukiboresha kikosi chao.

"Tunasajili kwa maelekezo ya kocha Taoussi, tumemsajili mchezaji huyu na siyo mwisho, hatujamaliza kusajili, tunategemea siku chache zijazo tunatangaza mchezaji mwingine," alisema Zaka Zakazi.

Juzi, klabu hiyo ilitangaza kumsajili, Zouzou, ambaye mbali ya kuwa ni beki wa kati, pia anaweza kucheza beki wa kushoto.

Baada ya kutangazwa kusajiliwa na Azam FC, mchezaji huyo alionyesha kufurahishwa na kuwataka mashabiki wa klabu hiyo kukaa mkao wa kula.

"Ninayo furaha kujiunga na Azam, tutaonana hivi karibuni," alisema mchezaji huyo.

Wakati hayo yakiendelea, wachezaji wa timu hiyo wameanza mazoezi kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tulianza mazoezi tangu Jumatatu kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili, tunaendelea hivi na mazoezi, lakini kila baada ya wiki moja tutakuwa tunacheza michezo ya kirafiki.

Nia ni kuangalia jinsi gani tunapiga hatua. Huwezi kufanya tu mazoezi kila siku halafu hujui umefikia wapi, ndiyo maana kocha wetu akasema kuwa anahitaji kufanya mazoezi kila siku na kucheza mechi kila baada ya wiki hadi pale Ligi Kuu itaporejea tena mwezi Machi," alisema Zakazi.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, Azam ipo kwenye nafasi ya tatu kwenye msimamo ikikusanya pointi 36 baada ya kucheza michezo 16 na kushinda michezo 11, sare tatu huku ikipoteza mechi mbili.

## Hatima Yanga robo fainali Afrika leo

INATOKA UK. 24

kimekwenda safi, tunachosubiri ni dakika 90 tu za mchezo," alisema Kamwe.

Ikumbukwe kuwa, Al Hilal inacheza mechi zake nchini Mauritania kutokana na Sudan kukabiliwa na machafuko.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, amesema mchezo wao dhidi ya Yanga siyo muhimu sana kwao, lakini anategemea kupata upinzani mkali kutoka kwa wapinzani wao kwa kuwa ni mchezo wanaouhitaji kupata matokeo mazuri.

"Niwapongeze wachezaji wangu kwa kazi ngumu na kubwa waliyoifanya katika michezo ya mwanzo, naamini tulitumia nguvu kubwa tofauti na michezo tunayoenda kucheza sasa presha itakuwa kwa wapinzani wetu.

Niseme tu kuwa, Yanga ya msimu uliopita siyo kama ya msimu huu, ubora wao umepungua, sisi tumefuzu, hatima yao ipo mikononi mwetu wafuzu au tuwatoe klabu bingwa.

Malengo yetu ni kumaliza tukiongoza kundi haitokuwa mechi rahisi kwao, wajipange," alisema Ibenge, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

## Simba kurudia ya 1993 Angola?

INATOKA UK. 24

kucheza na timu ambayo ni nzuri ikicheza kwao. Ni hatari mno inapocheza uwanja wao wa nyumbani na hata mechi zote ilizoshinda ilicheza hapo.

Tunatakiwa kucheza kwa umakini, tunatakiwa tuwe waangalifu, tukiwa na mpira na kipindi ambacho hatuna, kwa maana hiyo tunakwenda kucheza kimkakati, nia ni moja tu tusipoteze mchezo, tushinde au tupate sare, kwa sababu wanapenda zaidi kushambulia, wanafunguka na ndiyo maana inafunga mabao mengi. Lakini sisi hatuingii kwenye mtego huo, hatuwezi kufunguka kama wao wanavyocheza na kupishana nao, ila hatutowapa nafasi ya kuumiliki mpira, na tutatumia nafasi ambazo wao wanaziacha kuwashambulia," alisema Fadlu.

Kocha wa Bravos do Maquis, Mario Soares, amewaonya wachezaji wake kuwa makini kwenye mchezo huo, kwani wapinzani wao wana wachezaji ambao wana uwezo wa kuimaliza mechi.

„Inawachezaji wazuri, ni ngumu kumtaja kila mmoja kwa jina, ila mmoja wao ni yule mwenye jezi namba 10 (Jean Ahoua), kwangu huyo ndiyo hatari zaidi, anacheza taratibu tu, lakini mipira yake ni hatari sana," alisema kocha huyo.

Simba yenye pointi tisa, inahitaji angalau sare ili kuweza kutinga hatua ya robo fainali, huku Bravos do Maquis ambayo ina pointi sita, inahitaji ushindi ili ifikishe pointi tisa, halafu isubiri mchezo wa mwisho ugenini dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia.

Michezo
Jumamosi Januari 11, 2025
Nipashe

**Rashford kubadilishana na Kvaratskhelia wa Napoli** UKURASA 21



# Hatima Yanga robo fainali Afrika kesho

## ●●●Wawakilishi hao wa Tanzania wanahitaji ushindi tu huku wakiombea...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema amewaandaa wachezaji wake kimwili, kiakili na kiufundi kwa ajili ya mchezo wa raundi ya tano, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, utakaopigwa leo saa 4:00 kwenye Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott, nchini Mauritania.

Akizungumza akiwa nchini humo, Ramovic, alisema mchezo wa kesho ndiyo unashikilia hatima yao na wamejiandaa kuhakikisha wanashinda ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye mchezo wa mwisho utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya MC Alger ya Algeria, Januari 18, mwaka huu.

"Kwa sasa hatuwezi kuangalia matokeo ya mechi zingine, tunachotakiwa ni sisi wenyewe kuangalia kwanza tunafanya nini. Tunahitaji ushindi kwa hali na mali kwenye mchezo huu. Tukishinda tutakuwa na pointi saba ambazo zitatusogeza na kuangalia nini tutafanya katika mchezo wa mwisho," alisema kocha huyo.

Matokeo yoyote tofauti ya ushindi, yanaweza kuiweka kwenye hali ngumu zaidi Yanga ya kusonga mbele kwenye hatua ya robo fainali.

"Nimewaandaa vijana wangu kimwili, kiakili na kiufundi kwa ajili ya mchezo huu na wachezaji wanajua kuwa wanapaswa kushinda tu kama wanataka tusonge mbele," alisema kocha huyo.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe alisema tangu watue nchini humo hawajapata usumbufu wowote au dalili ya kuonyesha kuwa kuna hujuma dhidi yao, huku akisema hali ya hewa ni baridi ya kawaida ambayo haiwezi kuwazuia kucheza kwa ubora wao.

"Hakuna baridi ya kutisha kama ya Tunisia au Algeria, hatujagandishwa sana Uwanja wa Ndege, au kufanyiwa hujuma yoyote, kusema kweli kila kitu

INAENDELEA UK. 23



Sead Ramovic

# Simba kurudia ya 1993 Angola?

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Simba kesho saa 1:00 usiku kinatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Novemba 11, Luanda, Angola kufanya kile ilichokifanya miaka 31 iliyopita ilipofanikiwa kufuzu hatua ya fainali ya Kombe la CAF, ambalo sasa linaitwa Kombe la Shirikisho, dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao, ikiwa ugenini.

Simba itacheza mechi ya raundi ya tano, Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi dhidi ya Bravos do Maquis ya nchini humo katika mchezo ambao inahitaji ushindi au sare ili kufuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi A.

Kama itafanikiwa kufanya hivyo, itakuwa ni mara ya pili kwani mwaka 1993, Simba ilifanikiwa kuingia hatua ya fainali ya Kombe la CAF, ilipotoka suluhu dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao ikiwa nchini humo, katika mchezo wa marudiano baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Taifa Dar es Salaam (sasa Uhuru), Simba kupata ushindi wa mabao 3-1.

Iwapo itapata ushindi pia itakuwa ni mara ya pili kwani ikiwa nchini humo, Oktoba 9 mwaka 2022, iliichapa Primeiro de Agosto mabao 3-1, katika mchezo wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa huku wa marudiano uliochezwa nchini, Oktoba 16, 2022, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ilishinda bao 1-0, na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema maandalizi yote ya mchezo huo yamekamilika huku akisema atakwenda kuikabili Bravos do Maquis kwa mfumo tofauti.

Alisema kuwa timu hiyo ni hatari inapokuwa nyumbani, ikipenda zaidi kumiliki mpira, hivyo ametengeneza mkakati wa kuhakikisha wanawanyima fursa hiyo.

"Mechi itakuwa ngumu, inatakiwa tucheze kimkakati, tunakwenda

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042